# Nipashe

Jumatatu Januari 22, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581563

www.ippmedia.com

MWANG A JAMII



LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/thegu




**UMMY:** Ole wao watakaozuia maiti kisa deni hospitalini

UKURASA 8

**MAKONDA** amtaka 'kigogo' wa CCM akabidhi nyumba aliyonyang'anya

UKURASA 3

**JWTZ** yaonya askari wake unyanyasaji wa kingono

UKURASA 5



**ANGOLA ITAFUZU 16 – BORA: PEDRO**

UKURASA 22

## Wazazi waliolipa michango shuleni kurejeshewa fedha UK. 3

# TUTAJUTA

**MMOMONYOKO** wa maadili wamshtua Rais, awapa kazi viongozi wa dini; Papa amwalika Vatican...

*Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimpongeza Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Alex Malasusa, baada ya kuingizwa kazini wakati wa ibada maalum iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Azania Front jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



# MAFURIKO DAR

**ASIMULIA** maji yalivyochukua uhai wa mtoto wa jirani yake...

UKURASA 2

Wakazi wa Tegeta Machinjioni, wilayani Kinondoni, wakiokota matofali yaliyobomoka kwenye nyumba yao kutokana na mvua inayoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: ELIZABETH ZAYA**

**MICHEZO** KOCHA ASEMA TUNISIA HAIKUWA NA BAHATI UK. 22

**KATUNI** UK. 6

# Asimulia maji yalivyochukua uhai wa mtoto wa jirani yake

**Na Elizabeth Zaya**

"WAKATI nimetoka nje kukinga maji, niliona maji yanakuja kwenye eneo letu la nyumba kutoka mtoni, lakini mimi niliendelea na kazi yangu nikijua yanakuja na kuondoka kama ambavyo hupita siku nyingine."

Ni simulizi ya mkazi wa Tegeta Machinjioni, aliyejitambulisha kwa jina moja la Mage ambaye alikumbwa na mafuriko na mtoto mmoja kusombwa na maji katika Mto Tegeta.

Anasimulia kuwa baada ya kukinga jaba lake alirudi ndani ili achukue ndoo nyingine, akaona wimbi kubwa zaidi la maji linakuja, akakimbilia ndani kuwachukua watoto wake, mama yake, mdogo wake na mtoto wa rafiki yake ili wakimbie. Wakati wanakimbia kutoka, mlango ukabana ukagoma kufunguka na maji yakawa tayari yameanza kuingia ndani. Ikabidi ageukie upande wa dirisha ambako kulikuwa hakuna maji ili awatoe watoto, akafanikiwa kumtoa mmoja, kabla hajamtoa mtoto mwingine wa pili, maji yakajaa zaidi ndani akaona wanakufa, ikabidi apande dirishani atoke akawaite majirani maana wakati huo alikuwa akipiga kelele, lakini hakuna aliyeitikia.

Alifanikiwa kutoka na kumchukua mtoto aliyekuwa ameemtanguliza kupitia dirisha la nyuma ya nyumba, akakimbilia kumwita jirani, wakati huo ndani alikuwa amebaki mama yake, mdogo wake na watoto wawili mmoja wa kwake na mwingine wa rafiki yake. Walianza kuhangaika ili wavunje ukuta upande wa dirisha watoke.

Wakati wanahangaika kuvunja ukuta, mama yake alikuwa amembeba mtoto wa rafiki yake na mdogo wake alimbeba mtoto wake mwingine aliyekuwa amebaki, lakini bahati mbaya kabla hawajafanikiwa kuuvunja, ukuta ukameguka... kwa sababu walikuwa wameushikilia, mama yake na mtoto wakadondoka, mtoto akasombwa na maji, lakini mama yake akafanikiwa kushikilia tawi la mti, hapo kila mtu alikuwa anahangaika maji yakawashinda. "Tukapiga kelele jamani tusaidieni mtoto anaondoka na maji, lakini ndio akawa ameenda." Mage anasema mtoto aliyefariki alikuwa wa rafiki yake mwenye umri wa miaka sita na alikuwa akisoma katika Shule ya Msingi Kunduchi, Kinondoni. "Nachanganyikiwa zaidi, watoto wangu wawili wamenusurika, lakini mtoto wa rafiki yangu ndiye akasombwa, naumia sana. Ninaomba jamii isinihukumu, hata mimi sikutarajia kama hili lingetokea," anasema kwa uchungu Mage.

Kabla ya siku ya mvua iliyosababisha maafa hayo, Januari 19 alikwenda kwa rafiki yake mwenye mtoto aliyefariki kuwasalimia na wakati anaaga kurudi nyumbani kwake, mtoto huyo alianza kulia akitaka aende naye nyumbani kwake na hivyo akakubaliwa.

"Mtoto wangu na mtoto huyo aliyefariki walikuwa ni marafiki, kwa hiyo mara nyingi walikuwa wanatembeleana na kama siku ambazo hakuna shule, mmoja anaweza kwenda kwa mwenzake akalala huko halafu akarudishwa siku nyingine, ndivyo ilivyokuwa kwa huyu mtoto wa rafiki yangu (ambaye amefariki), baada ya kulilia twende naye tulikubaliana kwamba tumrudishe kesho yake, lakini sielewi hiki kilichotokea." Charles Paul, mkazi wa Tegeta aliyeuona mwili wa mtoto huyo na kuita majirani baada ya kuuokoa, alisema akiwa mtoni kushangaa namna mto ulivyofurika, aliona mkono ukiwa unaelea karibu na mti na kuamua kusogea na ndipo alipobaini kwamba alikuwa ni mtu.

"Baada ya kuona vile nilikimbia haraka ili kama hajafariki nimwokoe, lakini haikuwa bahati nilifanikiwa kumtoa na nikaita majirani, kinamama wakaja na kanga kumfunika wakasema amefariki ndipo ikabidi tupige simu kwa viongozi wa mtaa na wao wakaita Jeshi la Polisi na baadaye kututhibitishia kwamba alikuwa amefariki," alisema Charles.

Kaimu Mwenyekiti wa Mtaa wa Tegeta, Amos Mukamachuma, anasema alipewa taarifa za mwili kuokotwa kwenye mto huo, lakini baada ya kufuatilia wakabaini ni mtoto aliyefariki anatoka mtaa mwingine wa Tegeta Machinjioni.

Akizungumzia mtaa wake huo wa Tegeta, Amos alisema athari hizo za mvua pia zimekumba kaya zaidi ya 40 ambazo hazina sehemu ya kuishi baada ya nyumba tano walizokuwa wakiishi pamoja na mali zao kusombwa.

Balozi wa shina namba tatu wa Tegeta Msichoke katika mtaa huo, Salama Moshi, alisema kwa sasa msaada wanaopatiwa wakazi hao waliopoteza makazi yao ni kutoka kwa majirani wema ambao wanawasaidia chakula na sehemu ya kulala.

Nipashe ilishuhudia baadhi ya nyumba zikiwa zimezingirwa maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, huku miundombinu ya barabara na madaraja ikiharibika.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), lilitoa taarifa ya kuharibiwa kwa miundombinu kutokana na mvua iliyonyesha siku mbili mfululizo na kusababisha baadhi ya maeneo kukosa huduma ya umeme.



Daraja la Silva lililoko Tegeta lililovunjika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MAKTABA**

# Mmomonyoko wa maadili wamshtua Rais

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameziagiza taasisi za dini nchini kushirikiana na serikali kuziimarisha familia ambazo zinapitia changamoto nyingi za kimaadili, ikiwamo ndoa kuvunjika, vijana waliofikia umri kushindwa kuoa au kuolewa na kushamiri vitendo vya ukatili.

Alisema taasisi za dini zina mchango mkubwa wa kujenga familia zenye maadili kupitia mafundisho yenye kuimarisha kiroho na kutaka ziangalie ni wapi jamii ilipojikwaa na kurekebisha ili kujenga taifa lililoimarika.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam aliposhiriki ibada maalum ya kumwingiza kazini Mkuu Mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa.

Ibada hiyo ilifanyika katika Kanisa Kuu la Azania Front, Dayosisi ya Mashariki ya Pwani, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na dini.

Rais Samia alisema ripoti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuhusu Utafiti ya Ufuatiliaji wa Kaya ya mwaka 2022 inaonyesha kuwa zaidi ya nusu ya vijana waliofikia umri wa kuoa au kuolewa hawajaingia kwenye ndoa, huku wanaoishi mijini wakiongoza kwa asilimia 65 na vijijini asilimia 55.5.

Alisema kwa waliopo kwenye ndoa wanapitia changamoto mbalimbali zinazosababisha migogoro na kutoa mfano mwaka 2022/2023 kulikuwa na mashauriano ya migogoro ya ndoa 39,571 na nusu ya kwanza ya mwaka 2024 wameshapokea mashauri 28,773.

"Jambo hili inabidi tulitafakari kwa kina kama wanajamii kwani asilimia kubwa ya migogoro hii inahusisha ndoa za vijana au ndoa changa. Tunatoa fedha nyingi, masherehe makubwa, michango mingi baada ya mwaka, miaka miwili watoto kila mtu kwake," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema vyombo vya dini pia vina kazi kubwa ya kuwaponya na kuwaimarisha Watanzania kiroho ili kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia yanayozidi kuongezeka katika jamii.

Akirejelea taarifa ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2022 kuliripotiwa matukio 30,566 ya ukatili ikilinganisha na matukio 29,373 ya mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 4.1, huku waathirika wakubwa wakiwa ni wanawake na watoto.

"Haya yote yanatokea kwa sababu roho za watu zimeharibika, tunaishi kama ile hadithi ya shamba la wanyama, kila mmoja anamwinda mwenziwe. Tukiangalia namna taasisi za dini zote zinavyokuwa na matokeo haya haviendani, kwa hiyo lazima tujitafakari kama wanajamii na mchango wa vyombo vya dini," alisema.

Aliwasihi wazazi kuishi katika misingi ya kiroho wanayopewa na viongozi wao wa dini ili kuzinusuru ndoa zisivunjike, kwa kuwa kuna madhara makubwa kwa familia ikiwamo kuwapo watoto waliokosa misingi mizuri ya malezi na kuongezeka kwa watoto waliolelewa na watu wasio na nia njema kama aliyonayo mzazi kwa mwanawe.

Pia, aliwasihi wazazi katika nafasi zao za malezi kufuatilia mambo wanayoyafanya watoto wao katika mitandao ya kijamii, kuhakikisha kuwa wanahudhuria mafundisho ya dini kwa kuwa kinyume na hapo maadili yataendelea kuharibiwa.

"Tuwakamate watoto wetu waje kanisani, wapate mafunzo ya dini, watoto wa kike na wa kiume, kwa sababu kupitia dini ndiyo tunapata miongozo ya kimaisha. Kama wote tungefunzwa miongozo ya kimaisha yanayotokea sasa yasingekuwapo," alisema Rais Samia.

Alisema kwa kutambua changamoto hiyo mwaka 2022 serikali iliunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi maalum ambayo inaendelea kukabiliana na athari hasi zinazojitokeza katika jamii.

Rais Samia alisema serikali ina jukumu la kudumisha amani ya nchi ndiyo maana imekuja na R nne ambazo kwa Kiswahili ni mageuzi, maridhiano, ustahamilivu.

Kadhalika, alimpongeza Askofu Dk. Malasusa kwa kuchaguliwa kuwahudumia waumini wa KKKT na serikali itampa ushirikiano wa dhati katika kipindi chote cha uongozi wake.

Askofu Dk. Malasusa alimshukuru Rais Samia kwa kutenga muda wake na kuhudhuria misa hiyo hali inayoonyesha namna anavyoliheshimu kanisa.

Alisema hali hiyo inaonyesha mfano kwa mataifa mengine namna serikali na taasisi za dini zinavyoweza kushirikiana kwa upendo na amani katika mambo mbalimbali.

Aliiomba serikali kuziachia taasisi za dini kushughulika na suala la ndoa ya jinsia moja kwa kuwa hata vitabu vya dini vinaelekeza kuwa ndoa ni kati ya mume na mke na si vinginevyo.

Vilevile, aliwakumbusha Watanzania kuheshimu uumbaji wa Mungu wa jinsia ya kike na kiume na kuwa anayekwenda kinyume na hilo anakiuka misingi ya dini yake.

Akizungumzia nafasi aliyopewa na kanisa hilo, alisema atawahudumia kwa unyeyekevu akiamini kuwa Mungu ndiye aliyemchagua.

Aliwaomba maaskofu, viongozi wa dini na waumini waendelee kumwombea na kushirikiana naye katika kulinda umoja wa kanisa hilo kwa kuwa ndivyo Yesu Kristo anavyotaka.

Naye Mkuu wa KKKT mstaafu, Askofu Dk. Fredrick Shoo, alimpongeza askofu huyo kwa kuchaguliwa kuliongoza kanisa hilo kwa mara nyingine akiamini kuwa uwezo mkubwa alionao ndio umemfikisha hapo alipo.

Wakati huohuo, Rais Samia amepata mialiko ya kufanya ziara za kikazi katika maeneo matatu ikiwamo Vatican ambako amealikwa na Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, Februari 11 hadi 12.

Vilevile, Rais Samia atafanya ziara ya kikazi katika nchi ya Norway, Februari 12 hadi 13, pamoja na nchi ya Indonesia kuanzia Januari 24 hadi 25.

***Imeandaliwa na Jenifer Gilla na Maulid Mbaga**

# Wazazi waliolipa michango shuleni kurejeshewa fedha

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHULE ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga imeanza kuwarudishia wazazi fedha za michango Sh. 80,000 ambayo walilipishwa licha ya serikali kupiga marufuku michango shuleni.

Kuanzia Januari 2016, serikali ilipoanza kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimsingi Bila Ada, maarufu Elimu Bure, ada na michango mingine ya lazima shuleni ilizuiwa kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne.

Hata hivyo, iliripotiwa na gazeti hili wiki iliyopita kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga ilikuwa inatoza michango yenye jumla ya Sh. 80,000 kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alikemea kitendo hicho.

Kutokana na onyo hilo la waziri, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, akizungumzia hatua walizochukua, aliwaambia waandishi wa habari mjini Shinyanga juzi kuwa ufuatiliaji wao umebaini wazazi wamelipa fedha hizo isivyo halali.

Kati ya michango hiyo, Sh. 65,000 ni kwa ajili ya uendeshaji wa shule na Sh. 15,000 ya tahadhari, nembo na kitambulisho cha shule.

Alisema wakati wa uchukuaji fomu za kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hiyo, wazazi walichanganya wakachukua fomu ya kidato cha tano ambayo ndiyo ina michango hiyo ya Sh. 80,000 na kuacha ile ya kidato cha kwanza ambayo haina michango.

Mkurugenzi huyo alisema fomu za kujiunga na shule hiyo hazitolewi shuleni, bali kwenye mitandao ndiyo maana wazazi walichanganya na kuchukua fomu ya kidato cha tano yenye michango ya Sh. 80,000

Hata hivyo, tangu serikali ilipotanua Mpango wa Elimu Bure hadi kidato cha sita kuanzia mwaka wa fedha 2022/23, michango ya aina hiyo pia ilizuiwa kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Serikali inatoa ruzuku maalum ya uendeshaji wa shule kila mwezi. Hivyo, shule hiyo ya Shinyanya kuwatoza wanafunzi wa kidato cha tano si sahihi.

Mkurugenzi huyo alisema ameshamwagiza Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Nurah Kamuntu, arejeshe fedha hizo kwa wazazi.

"Baada ya taarifa kutoka kwenye gazeti Nipashe juu ya Shule ya Sekondari ya Wasichana kutoza michango iliyopigwa marufuku, ilibidi nifuatilie kwa kina na kubaini wazazi walichanganya uchukuaji fomu, badala ya kuchukua ya kidato cha kwanza ambayo haina michango, watachukua ya kidato cha tano iliyo na mchango wa Sh. 80,000.

"Tayari kiasi cha fedha Sh. milioni 4.475 ambacho kilikuwa kimeshatolewa na wazazi kupitia mchango huo wa Sh. 80,000 kimetolewa kwenye akaunti na shule na baadhi ya wazazi wameshaanza kurudishiwa fedha zao, wengine wanachukua cash (fedha taslimu) na wengine kutumiwa kwenye simu."

Alisema licha ya kuwapo mchango huo wa Sh. 80,000, wanafunzi walikuwa wanapokelewa na kuendelea na masomo huku wengine wakiwa hawana hata sare za shule.

Alibainisha kuwa ufuatiliaji wao umebaini kuwa hadi kufikia juzi Jumamosi, wanafunzi 100 walikuwa wamesharipoti shuleni huko kati ya 143 waliopangwa kujiunga na shule hiyo ambayo ni zao la mkakati wa serikali wa kuinua wasichana kupitia masomo ya sayansi.

Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Nurah, alisema baadhi ya wazazi wamesharudishiwa fedha walizolipa kama michango. Wengi wao wanachukua mkononi na wengine kutumiwa kwenye simu zao.

Mmoja wa wazazi hao, Ibrahimu Lyanga, alikiri kurejeshewa Sh. 80,000 aliyolipa shuleni huko kupitia michango ya lazima iliyokuwa imewekwa.

Alishukuru serikali kwa mpango wake wa kutoa elimu bila ada, akisema michango hiyo iliwashtua, lakini sasa wanashukuru makosa yalirekebishwa.

**WAZIRI AONYA**

Wakati hatua hizo zikichukuliwa Shinyanga, Waziri Mchengerwa alisema alionya juzi kuwa atachukua hatua kali ikiwamo kuwaondoa wakuu wa shule na maofisa elimu watakaoendekeza michango shuleni.

Alisisitiza kuwa tayari serikali imeshalipa ada kwa ajili ya wanafunzi wa shule za awali hadi kidato cha sita, hivyo hakuna sababu ya mtoto kurudishwa kwa kisingizio cha michango.

"Ninarudia nikisikia mkoa wowote, wilaya, halmashauri, mkuu wa shule ametataa kupokea watoto kujiunga na shule kwa sababu ya michango na kuleta kero kwa wananchi, mkuu wa shule huyo, ofisa elimu nitawaweka kando mara moja," alionya.

Alibainisha kuwa kwa sasa serikali inatoa wastani wa Sh. bilioni 33.3 kila mwezi kugharamia Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada.

***Imeandaliwa na Marko Maduhu (SHINYANGA) na Beatrice Shayo (BAGAMOYO)**

# Makonda aagiza kigogo CCM akabidhi nyumba aliyoipoka

**Na Beatrice Shayo,** TANGA

MWENYEKITI wa Wilaya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanga Mjini, Meja mstaafu Khamis Mkoba, ametakiwa kurejesha haraka nyumba anayodaiwa kumpora mwanachama wake, Nassor Fereji, aliyekuwa amewaazima ili kuendesha shughuli zao.

Paul Makonda, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, alitoa maelekezo hayo jana alipozungumza na wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, akiwataka viongozi hao kufungua ofisi jana na kutoa huduma baada ya kubaini kuwapo changamoto nyingi ikiwamo migogoro ya ardhi.

Fereji alisema nyumba yake aliombwa na Meja mstaafu Mkoba kwa kuwa iko jirani na CCM kwa madai wanataka waweke makatibu wao, alikubali kwa sababu yeye ni mwanachama wao.

"Mimi kwa sababu ni mwanachama wa CCM nikasema 'sawa, hakuna shida, makatibu ni wetu'. Nikatoa hiyo nyumba yenye ofa ya miaka 21 ambayo alikuwa nayo mmiliki wa kwanza, nikauziwa. Nimekaa nayo miaka 11 mpaka leo hii ofa yangu inaonyesha ni miaka 33.

"Mwaka jana nikaona wanaanza ujenzi wa matofali katika banda la uani, nikamfuata mwenyekiti nikamwuliza 'vipi'? Akanijibu 'hii yetu bwana, si yako tena'.

Nikamwambia inakuwaje mimi mwanachama wa CCM hivi kimnyang'anye nyumba mwanachama wake? Nikamwambia 'hiki si chama ni wewe!' Chama hakiwezi kufanya hivi," alisema Fereji.

Alidai kuwa alilazimika kwenda Idara ya Ardhi kuhakiki hati yake kujua kama iliibwa au la, akajulishwa namba 62 ni nyumba yake, akatakiwa kuonesha ofa yake na akatakiwa kueleza tatizo.

Makonda baada ya kusikiliza, alimuuliza "aliyekwambia hiyo nyumba si yako ni nani? Je, yupo hapa?

Katibu wa Wilaya unamjua aliyemtaja? Ina maana ni Mwenyekiti wa hii Wilaya ya Tanga? Duuu... ndio amechukua hiyo nyumba?

"Katibu una dakika mbili kuongea naye na kumtafutia mwenyekiti akabidhi nyumba yake leo (jana)," Makonda alielekeza huku akishangiliwa na wananchi.

**'DED ASIMAMISHWE'**

Akiwa wilayani Muheza, Makonda alisema kuwa wakati anatoka wilayani Pangani, alikuta kero nyingi alizodai zinasababishaa na mkurugenzi na akiwa njiani alimpigia simu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) akamjulisha mapendekezo ya CCM, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Pangani, Isaya Mbenje, asimamishwe kazi.

Pia alielekeza wenyeviti wa CCM katika wilaya zote nchini watoe ripoti za wakuu wa wilaya na wakurugenzi ambao ni wazembe katika wilaya zao.

Makonda pia alimpa miezi mitatu Meya wa Jiji la Tanga kuhakikisha wananchi 55 waliotolewa kwa ajili ya kupisha stendi ya mabasi Kange wanalipwa fidia iliyobaki ya Sh. bilioni 1.7. Ilitakiwa kutolewa tangu mwaka 2015.


**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**KENEDY LUCAS BARNABA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 347340** iliyotolewa makao makuu mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SON/MBO/269/2024**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 4(1&2(b)) ya Kanuni za Mafuta (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) ya Mwaka 2018**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya **Shirika la Maendeleo la Mafuta Tanzania (TPDC)** kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa njia ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa kilomita 2.648 kutoka BVS Na.13 hadi kiwanda cha KEDA kilichopo Kisiju Mkuranga, Pwani.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http./www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

217794302

Air Tanzania
Training Centre




KOZI YAWAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Center ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 01 Machi 2024. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam(JNIA) Terminal One kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwahapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Januari 2024

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Muomaji asiwe na michoro yoyote ya kudumu inayoonekana mwilini (visible tattoo)
iii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 (162 cms) na kuendelea
iv. Elimu sio chini ya kidato cha nne na kufaulu angalao masomo manne, hasa masomo ya Kiingereza na Jiografia
v. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
vi. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

**Angalizo:** Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kulinganisha matokeo ya vyeti vyao kwenye Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE) yafanane na matokeo ya Tanzania.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na vyeti vingine vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Mkuu wa Chuo,**
**ATCL Training Center**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam**
**Email, training@airtanzania.co.tz**

**Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali piga namba hizi TU:**
**Mob: +255754 345 874, +255735 787212**

ATCL TRAINING CENTER
"FULFILL YOUR FLYING DREAMS WITH US"


# Rais wa Barrick akabidhi jengo la abiria Uwanja wa Ndege Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

RAIS na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick Duniani, Dk. Mark Bristow, amekabidhi jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kahama, mkoani Shinyanga liliojengwa kwa Sh. milioni 896.7 na kampuni hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanda vya Ndege nchini (TAA).

Dk. Bristow alikabidhi jengo hilo jana kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga baada ya ujenzi ulioanza mwezi Machi, mwaka jana na kukamilika Novemba 30, 2023 likijengwa na Kampuni ya Umoja na Sons ltd.

Mtendaji huyo aliwataka viongozi wa mkoa huo kutumia jengo hilo kutangaza bidhaa zinazozalishwa mkoani humo ikiwa ni pamoja na kahawa itayotumika kwa abiria wanaosubiria usafiri ni inayozalishwa nchini na kuwataka viongozi wa mkoa kutumia jengo hilo kutangaza aina ya mazao ya chakula na biashara yanayozalishwa na wakulima.

Alisema, Sh. milioni 896.7 zimetumika kujenga jengo hilo kati ya hizo, Sh. milioni 615.8 zimetolewa na Barrick Buzwagi na Sh. milioni 256.7 kimetolewa na serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini (TAA) na kuwataka kuboresha njia ya kurukia ndege kuwa ya kiwango cha lami ili kipindi cha mvua ndege ziweka kushuka.

Aidha, alisema mgodi huo kabla ya kufunga uzalishaji ulikuwa kitovu cha uchumi mkoani Shinyanga kwa takribani miaka 15 na ulikuwa mgodi wa pili kwa ukubwa Tanzania na uliajiri zaidi ya watu 3,000 na ulifika tamati ya kuzalisha tangu mwaka 2021 na kufungwa mwaka juzi 2022.

"Jukumu la kampuni endelevu ya uchimbaji wa madini si tu kutengeneza thamani kwa wadau wakati uliopo, bali ni kuhakikisha kuwa inaacha urithi mzuri ambao utaendelea kuhudumia jamii kwa muda mrefu baada ya uchimbaji kufikia mwisho na sasa tunakabidhi jengo la kisasa litakalotumika na abiria wanasubiria usafiri wa anga," alisema Dk. Bristow.

Akipokea jengo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alipongeza kampuni hiyo kwa kutumia sehemu ya mapato yao kujenga jengo la kisasa la abiria ambalo litakuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 na kuwataka TAA kulitunza ili kuwa na kumbukumbu ya mgodi huo kwa kile ilichofanya baada ya kufunga uzalishaji.

Hata hivyo, alimwomba rais huyo kutuma timu na kwenda kufanya utafiti wa madini katika Wilaya ya Kishapu ili kuendelea na uchimbaji wa madini, kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga una maeneo makubwa yenye madini na yanahitaji utafiti. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini, Hamis Amiri alisema, jengo hilo litakuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 wakati awali lilikuwa linabeba abiria 25 pekee na sasa wanajiandaa kujenga eneo la maegesho ya magari, samani za ndani, mifumo ya TEHAMA, mifumo ya ufuatiliaji usalama la uwanja, mitambo ya kisasa ya kukagua abiria na mizigo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara alisema, jengo hilo limeufanya uwanja wa ndege Kahama kuwa na daraja la tatu C na watahakikisha wanaongeza njia ya kurukia ndege kutoka kilomita 1.5 hadi mbili ili kuhakikisha ndege za ATCL zinafika pia.

Alisema, serikali inaendelea kuboresha viwanja vya ndege nchini na sasa ujenzi unaendelea mkoani Mara, Tanga, Tabora, Arusha na Rukwa na kwa kuwa Wilaya ya Kahama inapakana na nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Sudani Kusini na DRC Kongo, uchumi utaongezeka na maendeleo pia.

# Wanafunzi wapewa elimu lishe bora kuepuka magonjwa yasiyoambukiza

**Na Steven William,** MKINGA

WANAFUNZI kutoka shule za msingi na sekondari wilayani Mkinga na Wilaya ya Tanga Mjini wamepatiwa mafunzo ya ufahamu wa lishe bora.

Elimu hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki kwa wanafunzi 1,000 kutoka shule 20 za msingi na sekondari.

Meneja Mwandamizi kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Nutrition Connect Tanzania, Andreas Mtita, alisema hayo alipokuwa akiwafundisha wanafunzi wa klabu za lishe kwenye shule mbalimbali za Wilaya ya Mkinga kupitia ufadhili wa Shirika la World vision Tanzania, mradi wa Mkinga.

Alisema vijana wengi wanatumia vyakula vinavyosababisha tatizo la kupatwa magonjwa ikiwamo shinikizo la damu na kisukari.

Alisema vijana wa rika la balehe wapo hatarini kupata magonjwa yasio ya kuambukiza ikiwamo shinikizo la damu kwa kushindwa kufuata utaratibu wa mlo kamili ambao umekuwa ukishauriwa na wataalamu wa masuala ya lishe.

Meneja wa World Vision Tanzania Mradi wa Mkinga, Evodia Chija, alisema wanafunzi wa sekondari na msingi zaidi ya 1,000 wa klabu za lishe shuleni watanufaika na elimu hiyo na wao kuwa mabalozi wa masuala ya lishe kwenye jamii na kusaidia kuepuka magonjwa yasiyo ambukiza.

Ofisa Lishe Wilaya ya Mkinga, Ernesta Mallya, alisema vijana balehe wanashindwa kutimiza mlo kamili kutokana na kuiga maisha ya mitandaoni ambayo ni hatari kwa afya zao.

Aliwataka wanafunzi hao kuzingatia masuala ya vyakula ambavyo husaidia kinga za mwili katika kukabiliana na magonjwa.

Wanafunzi Mariamu Abdallah na Salimu Singa pamoja na mwalimu anayesimamia klabu za lishe katika Shule ya Sekondari Mtimbwani, Shabani Gwaho, wamepongeza wadau wa shirika hilo na Nutrition Connect Tanzania kwa kuhakikisha wao wamekuwa wanufaika wa elimu ya masuala ya lishe na kuwa chachu ya kuendelea kufanya vizuri.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akiwa katika ziara ya kutembelea eneo la Mto Zira katika Kijiji cha Ifumbo wilayani Chunya, mkoani Mbeya ili kukagua hali ya mazingira ya mto huo unaokabiliwa na changamoto za kimazingira kutokana na uchimbaji wa madini uliofanyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JWTZ yaonya askari wake unyanyasaji wa kingono

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limesema halitomvumilia askari wake atakayejihusisha na vitendo vya unyanyasaji wa kingono ndani na nje ya nchi, wakiwamo wale wanaokwenda kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani kwenye mataifa yaliyokumbwa na machafuko ya kivita.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Salim Hajji Othuman wakati akizindua mafunzo ya siku 10 ya maofisa na askari wanaotarajiwa kwenda kwenye ulinzi wa amani nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) katika Chuo cha Mafunzo ya Ulinzi wa Amani Kunduchi jijini Dar es Salaam.

"Mkatekeleze majukumu yenu kwa kufuata sheria za jeshi letu, msiende kulitia aibu taifa, matendo ya unyanyasaji kingono huko ni kosa," alionya Mnadhimu Othuman.

Mkuu wa Tawi la Operesheni ya Mafunzo, Meja Jenerali Ibrahim Muhona, alisema JWTZ imeongeza mafunzo ya unyanyasaji wa kingono ili askari waweze kujiepusha na matukio.

Alisema jeshi limelazimika kufundisha somo hilo kwa lugha ya Kiswahili ili kuhakikisha kila mpiganaji anaelewa na kumsaidia kutii maelekezo na sheria zake.

Akifafanua zaidi, alisema JWTZ halina sifa mbaya linapokwenda kutekeleza majukumu yake, linazingatia misingi yote inayotakiwa.

Mkuu wa Kituo cha Mafunzo ya Ulinzi na Amani (PTC), Brigedia George Itangale alisema maofisa na askari wanaokwenda kwenye ulinzi wa amani ni waadilifu na ameiva kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Alisema JWTZ kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) huwa na utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya kinidhamu maofisa wake kabla ya kwenda kwenye operesheni za ulinzi wa amani.

# Zimamoto watoa ufafanuzi mapovu yaliyozua taharuki

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

TAHARUKI imejitokeza katika wakazi wa Mji wa Morogoro baada ya kuonekana mapovu makubwa meupe katika maeneo mbalimbali ya mji huo, hususani Kata ya Tungi, jambo lililowatia hofu.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya asubuhi baada ya mvua kubwa iliyoambatana na radi na upepo mkali kunyesha kwenye maeneo mbalimbali ya Mji wa Morogoro na watu kuhusisha hali hiyo na kuanguka kwa kitu kutoka mawinguni.

Mwandishi wa habari hizi alifika maeneo ya Tungi na kushuhudia povu hilo kubwa likiwa limetanda katika eneo moja likiendelea kusambaa kwenye mifereji ya maji.

Baadhi ya wananchi waliokuwa kwenye eneo hilo, wakiwamo Hidaya Said, Rehema Mkonje na Freddy Petter, walieleza kushangazwa na hali hiyo ambayo walidai toka wamezaliwa na kuishi huko, hawajawahi kuona hali hiyo.

"Ndio kwetu huku, hili povu linatisha kiukweli, sijawahi kuona maisha yangu yote, inawezekana ni mawingu," alisema Rehema Mkonje, mkazi wa Tungi.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, alidai povu hilo limetokana na kupita kwa lori lililokuwa limebeba kemikali ya kutengeneza sabuni na kupata ajali iliyosababisha kemikali hiyo kumwagika na kusababisha povu hilo lililoendelea kusambazwa na maji, ingawa ajali hiyo haikuonekana maeneo hayo.

Kutokana na taharuki hiyo iliyozusha sintofahamu si tu kwa wakazi wa Morogoro peke yake, bali pia kwenye mitandao ya kijamii, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro limetoa ufafanuzi kuwa kwa kawaida povu la maji katika maeneo ya mto husababishwa na kuoza kwa viumbe hai kama mimea au mwani ndani ya maji.

"Wakati nyenzo hizi za kikaboni zinavunjika (kuoza), hutoa 'compounds' inayoitwa 'surfactants' ambayo hupunguza mvutano wa maji.

"Upungufu huu wa mvutano wa maji husababisha kuundwa kwa povu, hali hii hutokea zaidi katika maji ya chumvi (bahari).

"Zaidi ya hayo, mambo kama vile mmomonyoko, mtiririko mkubwa wa maji, na kuwapo vichafuzi vya maji, vinaweza pia kuchangia kutokea kwa povu kubwa katika mto," jeshi hilo lilisema katika taarifa yake iliyotolewa na Sajenti Benjamin Bandula.

Taarifa hiyo ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ikataja maeneo mbalimbali yaliyopata mkusanyiko huo mkubwa wa mapovu kuwa ni Tubuyu Shule, Mafuruni, JKT Nanenane, kituo cha mafuta cha ATN, Tungi Makaravati na maegesho na eneo la kuoshea magari jirani na Chuo Kikuu cha Jordan.

"Mpaka kufikia majira ya ya jioni Januari 20, 2024 (juzi), hali hiyo imepungua na kupotea katika baadhi ya maeneo isipokuwa maeneo yenye makorongo na mtiririko wa maji mengi," jeshi hilo lilibainisha.

Jeshi hilo lilisema kuwa hakuna taarifa yoyote ya kutokea madhara kwa binadamu na mifugo iliyoripotiwa kutokana na kuwapo povu hilo katika mto na vijito mbalimbali.

Jeshi hilo liliwapa tahadhari wananchi na viongozi wa serikali za mitaa kuhusu hatua mbalimbali za kuchukua katika maeneo yanayopitwa na mto unaokwenda kuunganisha Mto Ngerengere kutokana na kutofahamika kwa chanzo halisi cha povu hilo, ikiwamo kutotumia maji hayo kunywa, kufulia wala kuoshea vyombo na matunda.

"Dalili zifuatazo zitaonekana kwa baadhi ya wananchi ndani ya saa 12, endapo mtu atatumia maji ya kunywa ama kuoshea vyombo na matunda pamoja na kula samaki wanaotoka katika mto na vijito vya mto husika ikiwamo kuumwa kichwa kuliko kawaida, macho kuwa mekundu kuliko kawaida, mwasho wa ngozi, koo na pua kufukuta.

"Pia kujawa mate mdomoni kusiko kawaida, kuumwa tumbo, kichefuchefu, kutapika ama kuharisha," alisema Sajenti Bandula katika taarifa yake.

Hata hivyo, kiongozi huyo alihadharisha kuwa hali hiyo inaweza pia kuwa imesababishwa na umwagaji au utiririshaji wa kemikali katika mto huo na kwamba watu wenye magonjwa ya pumu, matatizo ya moyo na upumuaji huenda wakakumbwa na madhara makubwa zaidi endapo watatumia vitu vilivyohusiana na maji hayo yenye povu.


**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
S. L. P. 35928, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu: +255 22 2401581, Nukushi: +255 22 2401582
Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz Tovuti: www.thtu.or.tz

THTU

Tarehe: 22/01/2024

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu Tanzania (THTU) Kinakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi kama ifuatavyo;-

**1.0 CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU ZA JUU TANZANIA (THTU)**

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu Tanzania (THTU) ni miongoni mwa vyama vya wafanyakazi vilivyopo nchini kikiwa kimepata usajili Na. 23 mnamo tarehe 12/12/2008. Kwa mujibu wa katiba yetu, THTU inajumuisha wafanyakazi wa vyuo vikuu, Vyuo vikuu vishiriki (Umma na Binafsi), Taasisi za Elimu ya Juu zisizo vyuo vikuu pamoja na mamlaka zinazosimamia ubora na maendeleo ya elimu nchini Tanzania.

**2.0 MHASIBU – NAFASI 1**

**2.1 Sifa za Mwombaji**

i. Mwombaji anatakiwa awe na Shahada ya Uhasibu (Bachelor Degree in accountancy) au Stashahada (Postgraduate Diploma) ya Juu ya Uhasibu kutoka Chuo Kikuu/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali. Awe Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa mwenye cheti cha uhasibu cha CPA (T) kinachotambuliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), Mwenye ujuzi wa kutumia Kompyuta, uzoefu wa kazi utazingatiwa.

**3.0 KAZI NA MAJUKUMU:**

i. Kusimamia matumizi ya fedha za fungu lililotolewa.
ii. Kuthibitisha malipo ya aina zote.
iii. Kuandika taarifa ya mapato na matumizi kwa mujibu wa kanuni za Fedha na miongozo mbalimbali ya fedha ya nchi.
iv. Kutayarisha Hesabu za mfuko ama mifuko mbalimbali ya Chama inayoweza kuanzishwa kwa ajili ya shughuli maalum.
v. Kutayarisha hesabu za Chama
vi. Kufanya kazi yoyote atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi

**4.0 NGAZI YA MSHAHARA NA MUDA WA AJIRA**

Mshahara utakuwa kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa THTU. Hali kadhalika, ajira itakuwa ya kudumu kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa Chama.

**5.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 40.
ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza kwenye wasifu (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma na ujuzi.
v. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
vi. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", Hati Matokeo za Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.
vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 16 Februari, 2024 saa 10:00 jioni.
viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kupitia barua pepe ifuatayo: Barua Pepe: **generalsecretary@thtu.or.tz**

**IMETOLEWA NA:**

**Elia Kasalile,**
**Katibu Mkuu wa Chama**

217794202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Afcon darasa lingine kwa waamuzi wa Ligi Kuu Bara

**JUMATATU** iliyopita tulieleza hapa kufurahishwa na namna waamuzi waliochezesha michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar, walivyofanya kazi yao kwa usahihi hususan suala zima la utunzaji wa muda kwa kuhakikisha mpira unachezwa kwa dakika zote 90.

Katika michuano hiyo, ambayo ilifanyika Uwanja wa New Amaan Sports Complex mjini Zanzibar na Mlandege FC ikiibuka mabingwa kwa mara ya pili mfululizo, tuliweka wazi namna waamuzi walivyokuwa makini kuulinda muda unaopotezwa na wachezaji hususan kwa timu iliyombele kwa matokeo na kuufidia hata baada ya dakika za majeruhi kumalizika.

Tunaelewa na tumekuwa tukishuhudia baadhi ya wachezaji wamekuwa wakiutumia muda wa nyongeza kwa kujiangusha kuonyesha wamechezewa madhambi au kuchelewa kutoka pale kocha anapofanya mabadiliko, jambo ambalo humlazimu mwamuzi kuongeza muda zaidi baada ya ule wa nyongeza kumalizika.

Katika hilo, tuliwataka waamuzi wa Ligi Kuu Bara kujifunza kwa wenzao wa Zanzibar namna kanuni za sasa zinavyohitaji kuhakikisha mpira unachezwa kweli kwa dakika 90 na si kuacha wachezaji wajanja wajanja wautumie kwa kuupoteza.

Hata hivyo, pengine wapo waamuzi ambao somo hilo halikuwaingia vema, jambo ambalo tunazidi kuwakumbusha na kusisitiza fursa hiyo bado ipo kupitia Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazoendelea nchini Ivory Coast, Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, ikiwa miongoni mwa mataifa 24 yanayopeperusha bendera za nchi zao.

Katika fainali hizo za AFCON, tunaona namna waamuzi wanavyohakikisha mpira unachezwa kwa dakika zote 90 na hata zile za nyongeza zinapomalizika kama kuna muda ulipotezwa na haukutumika mpira ukiwa unachezwa, basi mwamuzi wa kati anachukua jukumu la kuufidia, jambo ambalo katika Ligi Kuu ni nadra kuona mwamuzi amefanya hivyo.

Tunaendelea kusisitiza kwa waamuzi kuzingatia hilo, lakini kwa mashabiki wa soka kutambua kwamba muda wa nyongeza unapomalizika kama hakutumika ipasavyo kwa mpira kuchezwa na badala yake baadhi ya wachezaji kuutumia kujiangusha angusha, kuchelewa kutoka wanapofanyiwa mabadiliko ama kwa namna yoyote ya kupoteza muda, jukumu la kuongeza hubaki kwa mwamuzi wa kati na anatakiwa kufanya hivyo bila kusikiliza kelele za mashabiki.

Mara nyingi waamuzi wa Ligi Kuu Bara wanashindwa kutii kanuni/sheria hiyo kwani dakika za nyongeza zilizooneshwa na mwamuzi wa akiba zinapomalizika, hapo hapo humaliza mchezo bila kujali kwamba muda huo ulitumika ipasavyo kwa mpira kuchezwa.

Lakini pia hata waamuzi wanaothubutu kuuongeza mashabiki hupiga kelele na kuelekeza shutuma kwao baada ya mechi kwamba waliibeba timu iliyokuwa nyuma kwa matokeo kwa kurefusha muda zaidi, jambo ambalo pia tunatamani kuwaona nao wakitumia michuano hii ya Afcon kujifunza ili kupunguza shutuma kwa marefa nchini.


Tunatambua si kwamba waamuzi wote wa soka nchini hawalifahamu hilo la kuhakikisha mpira unachezwa kweli kwa dakika zote 90 kwa kufidia zile zote zinazopotea mpira ukiwa umesimama, bali wengine huogopa presha kubwa kutoka kwa mashabiki ambao mara nyingine huwasababishia hadi kuchukuliwa hatua.

Hivyo, kama waamuzi na wapenzi wote wa soka nchini, hawataishia tu kuitazama michuano ya Afcon kujiburudisha, na badala yake kujifunza kitu, tunaamini tuendapo Tanzania itakuwa na ligi bora zaidi na kuvutia wengi kuwekeza katika sekta hiyo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Stars isibebeshwe mzigo mkubwa wa matarajio

Na Adam Fungamwango

**MASHABIKI** wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, wanaifananisha na kikosi cha Cameroon, Ivory Coast, Ghana, Mali, Burkina Faso, Senegal, Morocco na nchi nyingine nyingi za Kiafrika ambazo zimepiga hatua kubwa kisoka na kusahau bado inajitafuta.

Wanaiona Stars ikiwa kwenye levo za timu hizo, hivyo inapoingia tu uwanjani ishinde, bila kuangalia vitu vingi nje ya uwanja ambavyo vinasababisha timu inaingia uwanjani kwenda kumalizia.

Leo sitaki kuzungumzia kuhusu kufungiwa kwa Kocha Mkuu, Adel Amrouche, aliyefungiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), na Shirikisho la Soka nchini (TFF), nalo likapigilia nyundo hapo hapo kwa kumsimamisha na wasaidizi wake, Hemed Suleiman Morocco na Juma Mgunda wakichukua nafasi, ila nitazungumzia kuhusu mashabiki wanavyokuwa na matarajio makubwa na kikosi hicho kiasi cha kushindwa kujua uwezo halisi uko wapi.

Kitendo hiki ndicho kinachosababisha mashabiki kupiga kelele na kulalamika pindi timu inaposhindwa kupata matokeo mazuri.

Inawezekana wapo watu ambao wanatengeneza mazingira ya kuwafanya Watanzania kuiona timu yao ni kama Timu ya Taifa ya Misri hivi, haipaswi kufungwa na Morocco ambayo ndiyo timu pekee ya Afrika katika historia ya soka duniani iliyofika nusu fainali ya Kombe la Dunia.

Sisemi kama Stars haipaswi kushinda mechi yoyote ile ya fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), lakini mashabiki hawapaswi kutoa asilimia nyingi sana za kufanya vema zaidi kuliko uhalisia wenyewe.

Ukiangalia timu nyingi za Afrika Magharibi zina wachezaji waliotapakaa sehemu mbalimbali duniani kucheza soka la kulipwa tena kwenye klabu kubwa na maarufu Ulaya, lakini kuna baadhi ya nchi ambazo miaka ya hivi karibuni kama Cape Verde haikuwa juu sana kisoka, ila kwa sasa wanaonekana wapo mbali.

Nchi nyingi zina mipango sahihi ya kukuza soka la vijana, wachezaji wao kwenda kucheza soka la kulipwa na ushindani wakiwa bado na umri mdogo, uraia pacha, na vingine vinavyofanana na hivyo, vyote vikichanganyika vinazifanya timu nyingi kuwa bora kwenye AFCON.

Tanzania ndiyo kwanza imeanza kukusanya wachezaji kutoka nje ya nchi, ambao nao si kama wanacheza klabu kubwa sana Ulaya, hivyo bado ni kama inajikongoja, ikiendelea kuwategemea zaidi wale wale kina Mbwana Samatta, Simon Msuva, Dismas Novatus na wengine.

Badala ya kulaumiana, mara kocha, wachezaji, TFF, ili mradi kila mtu akitafuta yoyote wa kumtupia lawama, mimi nilidhani michuano hii iwe ni ya kujifunza zaidi badala ya kutaka timu ifike robo fainali. Ikifika hewala, lakini binafsi ninachowadai ni kupata ushindi wa kwanza kwenye fainali za AFCON tangu kuanzishwa.

Isiposhinda mechi yoyote hapo nitaona imefeli, lakini si matokeo mengine zaidi ya hapo.

Ikumbukwe kuwa Stars haijawahi kushinda mechi yoyote ya fainali za AFCON mara zote mbili ambazo imefanikiwa kuingia mwaka 1980 na 2019.

Ikiwa Kundi A, 1980 na timu za Ivory Coast, Misri na Nigeria ilimaliza ikiwa na pointi moja, ikicheza mechi tatu, ikipoteza mbili na sare moja ya bao 1-1 dhidi ya Ivory Coast na hayo ndiyo yalikuwa mafanikio makubwa zaidi kuyapata Stars kwenye michuano hiyo kabla ya mechi ya jana dhidi ya Zambia.

2019, ikiwa Kundi C na timu za, Kenya, Senegal na Algeria, ilipoteza mechi zote. Kwa maana hiyo haiwezekani itoke bila kushinda mechi yoyote ya makundi AFCON ifike nusu fainali, fainali na kuchukua kombe. Kila kitu kinakwenda kwa awamu.

Ili Stars ianze kufanya vema kwenye AFCON, ushindi kwenye hatua ya makundi kwake iwe jambo la kawaida.

Nachotaka kusema kuwa tuiunge mkono Timu ya Taifa ya Tanzania kwa sababu sisi ni Watanzania, lakini tusijipe presha zisizokuwa na sababu kiasi cha kuanza kuonyeshana vidole, badala yake ninavyoona kwa takwimu hizi tu, ushindi wa mechi moja tu AFCON itakuwa ni mafanikio makubwa kwa Stars kwa sababu itakuwa imeweka rekodi ambayo haikuwahi kuiweka huko nyuma.

HABARI KITAIFA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TCB, Adam Mihayo (kushoto), akipeana mkono na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba (kulia), baada ya kutembelea ofisi za Benki Kuu jijini Dar Es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NAM yaazimia kuimarisha uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Wakuu wa Nchi na Serikali Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) katika mkutano wa 19 uliomalizika juzi, Kampala, Uganda, pamoja na mambo mengine, wamekubaliana kuimarisha uwekezaji kwenye sekta mbalimbali ikiwamo ya viwanda ili kukuza uchumi.

Majaliwa ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano huo, aliyasema hayo juzi mjini Kampala, Uganda baada ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa 19 wa NAM ulioanza tarehe 15 - 20 Januari, 2024. Katika mkutano huo Rais wa Uganda, Yoweri Museveni alikabidhiwa uenyekiti wa NAM.

"Kwenye uchumi bado nchi wanachama tumesisitizwa uwekezaji kwenye viwanda, uwekezaji kwenye kilimo, uwekezaji kwenye maeneo yanayoweza kuboresha uchumi na hasa kuhamasisha wafanyabiashara wa ndani ya nchi hizo kujenga uhusiano na wafanyabiashara wa mataifa mengine kwa lengo la kuinua uchumi ili kujijenga zaidi," Majaliwa alisema.

Akizungumzia kuhusu masuala ya kijamii, Waziri Mkuu alisema nchi hizo zimekubaliana kuendelea kuzihamasisha jamii zao ziendelee kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii zikiwamo za kujenga uchumi, kulinda ulinzi na usalama katika maeneo yao na pale linapotokea wahakikishe wanayamaliza wenyewe ndani ya nchi zao.

Waziri Mkuu alisema katika mkutano huo pia wamekubaliana namna ya kushughulikia masuala ya kisiasa.

"Tumehitimisha kwa kutoa wito kwa nchi wanachama kila nchi ambayo imeweka utaratibu wake kisiasa waendelee na panapotokea kuwa na matatizo ya kisiasa, basi waendelee kuyatatua matatizo yao kwa kukaa kwenye meza ya mazungumzo na kuyamaliza," alisema.

Rais wa Uganda na Mwenyekiti wa NAM, Museveni, aliyataka mataifa yaliyoendelea yashiriki katika kukuza uchumi wa nchi zinazoendelea kwa kununua bidhaa kutoka katika nchi hizo pamoja kuwekeza kwenye sekta mbalimbali zikiwamo za viwanda na biashara.

"Wanachama wa NAM pamoja na changamoto za kimaendeleo zilizopo, bado tuna nafasi ya kuzikabili sisi wenyewe kwa kusaidiana katika masuala mbalimbali ikiwamo kufanya biashara baina yetu kwa kununua bidhaa kutoka kwenye nchi zetu kwani tunaidadi kubwa ya watu.

"Pia tuendelee kuweka mipango ya kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kuboresha miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa anga ili kurahisha ufanyaji biashara," alihimiza.

Awali Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutteres, alitoa wito kwa mashirika ya kimataifa na nchi zilizoendelea kuwa na mpango endelevu wa misamaha ya madeni kwa nchi za Afrika ili ziweze kuwa na maendeleo endelevu kwenye sekta za elimu, afya, nishati ya umeme pamoja na kukabiliana na baa la njaa.

Gutteres pia alizitaka nchi za magharibi ambazo ziliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kuzisaidia nchi za Afrika zinazokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, zitoe fedha hizo na mataifa wanachama wa NAM kuzikumbusha nchi hizo kutoa fedha hizo ndani ya mwaka huu.

Mkutano huo wa siku mbili ulianza Ijumaa, Januari 19, 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Ruwenzori, Speke Resort Kampala, Uganda.

Mkutano wa NAM hufanyika kila baada ya miaka mitatu na Mkutano wa mwisho, wa 18 ulifanyika jijini Baku, Azerbaijan mwezi Oktoba, 2019. Mkutano huo haukufanyika tangu mwaka 2019 kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 lililoikumba dunia.

Mkutano huo unalenga kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya biashara, uwekezaji, kutokomeza umaskini, mabadiliko ya tabianchi, amani na usalama katika mipaka, sekta ya afya, mandeleo endelevu na uchumi wa kidijiti.

Umoja huo ulianzishwa wakati wa enzi za vita baridi ili kusaidia nchi wanachama wake kutoka mabara ya Asia, Afrika na Latin Amerika kuondokana na ukoloni ili kuweza kujitawala kisiasa, kiuchumi na kijamii.

# Utafiti hali ya nguvu kazi sasa kufanyika kila mwaka

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi utakuwa unafanyika kila mwaka badala ya miaka mitano ili kuongeza kasi ya upatikanaji takwimu za soko la ajira nchini.

Hatua hiyo inatokana na kasi ya kukua kwa teknolojia na kuongezeka kwa utandawazi ambao umechochea kasi ya mabadiliko ya soko la ajira.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, wakati akifunga mafunzo kwa Wadadisi na Wasimizi wa Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2024 yaliyofanyika mjini Morogoro.

Mafunzo hayo ya utafiti huo yamehusisha wadadisi 139, wasimamizi 26 ambao ni mameneja wa takwimu wa mikoa, utafanyika kwa miezi 12 ili kuwezesha kupima kikamilifu mienendo ya ajira na ukosefu wa ajira kwa vipindi au misimu yote ya mwaka.

Alisema serikali inahitaji kupata takwimu za kina za soko la ajira zitakazoakisi hali halisi kwa ajili ya kufanya uamuzi wenye tija zaidi.

Prof. Ndalichako alisema lengo kuu la utafiti ni kupata viashiria vya soko la ajira nchini, kiwango cha ukosefu cha ajira, kiwango cha ajira isiyotimilifu, kiwango cha nguvu kazi, kiwango cha ajira mbaya kwa watoto na kiwango cha ajira kwa aina ya kazi.

"Taarifa hizi zitaisaidia serikali kufahamu hali halisi ya soko la ajira nchini ilivyo kwa kubainisha maeneo tunayofanya vizuri na maeneo yenye changamoto kwa ajili ya kuweka mikakati zaidi ya kukuza uchumi na ajira zenye staha," alisema Prof. Ndalichako.

Waziri huyo alisema mpango umelenga kuisadia serikali kuweka mikakati ya kufikia malengo iliyojiwekea ifikapo mwaka 2025 kuzalisha ajira milioni nane ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025.

Alisema mpango pia unadhihirisha dhamira ya serikali kuhakikisha inapanga mipango ya maendeleo kwa kuzingatia takwimu sahihi ili kukuza uchumi pamoja na soko la ajira.

Alisema kuwa kasi ya kukua kwa teknolojia na kuongezeka kwa utandawazi, imechochea pia kasi ya mabadiliko ya soko la ajira.

Alisema kutokana na umuhimu huo, serikali inahitaji kupata takwimu za kina za soko la ajira zitakazoakisi hali halisi kwa ajili ya kufanya uamuzi wenye tija zaidi.

Prof. Ndalichako alisema matokeo ya utafiti huo yatatumika kupima na kufuatilia utekelezaji mipango ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa.


Pia alisema matokeo ya utafiti huo yatasaidia kupima utekelezaji Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kwa Tanzania Bara na pia yatatumika kupima utekelezaji programu mbalimbali za kupima ukuzaji, ujuzi na uzalishaji wa fursa za ajira.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema utafiti huo utafanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa mikoa ya Tanzania Bara itafanyika kwenye maeneo 441 ambayo yamechaguliwa kitalaamu kuwakilisha maeneo mengine yote nchini.

Alishukuru wadau wa maendeleo ikiwamo Benki ya Dunia pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa ajili ya kufanikisha utafiti huo.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Tanzania Bara, Spika mstaafu, Anne Makinda, alisema takwimu zinaonesha asilimia 55.4 ya wananchi ni nguvukazi za Taifa, lakini hakuna uhalisia, hivyo kupitia utafiti huo utasaidia kuleta uhalisia ili kuisaidia serikali kufanya uamuzi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

DHAHABU MTONI

# Waziri atoa maelekezo kwa wawekezaji

**Na Robert Hokororo,** CHUNYA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo ameelekeza wawekezaji wote nchini kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kutekeleza mradi wowote ili kulinda mazingira.

Pia amewataka wachimbaji wa madini waliopata leseni za uchimbaji kutoka mamlaka husika kuanza zoezi la kufanya tathmini hiyo ili iwaelekeze namna ya kufanya shughuli zao bila kuathiri mazingira.

Alitoa maelekezo hayo alipotembelea eneo la Mto Zira katika Kijiji cha Ifumbo, wilayani Chunya, mkoani Mbeya ili kukagua hali ya mazingira ya mto huo unaokabiliwa na changamoto za kimazingira kutokana na uchimbaji wa madini uliofanyika.

Dk. Jafo alielekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhakikisha Kampuni ya G & I Tech Limited ambayo imekuwa inachimba dhahabu katika eneo hilo inafanya tathmini hiyo.

Alimtaka mwekezaji huyo kukamilisha mchakato wa TAM ambao utaainisha nini anachopaswa kufanya katika shughuli zake ikiwamo uchakati wa mchanga ufanyike nje ya mto na si ndani kwa kuwa kitendo hicho kinachangia uharibifu wa mazingira ya mto.

Pia alielekeza itumike teknolojia mbadala ya uchimbaji dhahabu ndani ya mto huo kuvuna dhahabu huku akishauri utungwe mwongozo wa usafishaji mito katika eneo hilo kuepusha uharibifu wa kingo za mto na mazingira kwa ujumla.

"Hatutaki kuzuia wawekezaji na tunatambua serikali imeendelea kufungua milango ya uwekezaji ili kukuza uchumi, lakini wawekezaji hao wanapaswa kuzingatia Sheria ya Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake ili kunusuru mazingira," alisisitiza Dk. Jafo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema Mto Zira ni tegemeo kubwa kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo, hivyo unapaswa kutoharibiwa mazingira yake.

Alisema wawekezaji wakiwekeza katika teknolojia, nchi itafanikiwa na madini yataendelea kupatikana, lakini uchimbaji ukifanyika kienyeji kutakuwa na athari.

Mkuu wa Mkoa Homera aliongeza kuwa serikali inatamani na kuthamini wawekezaji kwa kuwa wakiendelea kuwekeza inapata mapato na vijana wanapata ajira.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC, Dk. Thobias Mwesiga, alisema hatua za kufanya TAM kwa mwekezaji huyo zinaendelea kwa lengo la kumwezesha aendelee na uchimbaji.

Alisema ni kweli shughuli za uchimbaji zinaweza kufanyika kokote, lakini kinachoangaliwa zaidi ni kuzingatia wa sheria ili kujua madhara na maslahi yatakayopatikana kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya uwekezaji.

Dk. Mwesiga aliongeza kuwa kuna kipengele cha kuwashirikisha wananchi kwa asilimia zote kwenye tathmini ya athari kwa mazingira kinalenga kuhakikisha shughuli zinafanyika bila kuathiri mazingira.



Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wakisikiliza na kufuatilia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa katika kikao cha pili cha baraza hilo kilichofanyika mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ummy: Ni marufuku hospitali kuzuia maiti

**Na Beatrice Shayo,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amepiga marufuku ndugu kuzuiliwa kuchukua maiti katika hospitali zote za serikali nchini inapotokea wameshindwa kulipa gharama za matibabu.

Waziri Ummy alielekeza hayo juzi jioni mkoani Tanga katika ziara ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, aliyemtaka waziri huyo atolee ufafanuzi hoja za baadhi ya wananchi, wakiwamo waliodai kuzuiliwa kuchukua maiti hospitalini kwa kuwa wanadaiwa.

"Kwa kuwa wewe ni Waziri wa Afya, una mkakati gani wa kusaidia hasa pale mwananchi maskini anapompeleka mtu wake kumtibu na bahati mbaya anaitwa na Mungu?

"Mtu huyo anadaiwa kulipia maiti na wakati huo hana uwezo wa kutoa, hasa ndugu zangu wa imani ya Kiislamu inafika hatua wanashindwa kutimiza tendo la kiimani la kuwahifadhi na kuwasitiri ndugu zao kwa wakati kwa sababu hawana fedha za kulipa deni na kukomboa mwili.

"Kama waziri mwenye dhamana jambo hili ninajua umekutana nalo na linawakera Watanzania. Hata nilipokuwa Mwanza kwenye mkutano kama huu alijitokeza mwananchi analia maiti yao imezuiliwa pale Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Sekou - Toure).

"Mheshimiwa waziri unaweza kutueleza mkakati ulionao ili wananchi hawa ambao ni maskini wapate nafasi ya kusitiri ndugu zao badala ya kuichukia serikali ya CCM kwa kung'ang'ania miili iliyoshindwa kulipiwa baada ya kupoteza maisha?"

Akitolea ufafanuzi, Waziri Ummy ndipo akarejea tena maelekezo yake ya awali kwamba kwa hospitali zote za serikali, ni marufuku kuzuia maiti ya Mtanzania yeyote.

"Ninarudia, mara tatu ninasema, ni marufuku kuzuia maiti haya ni maelekezo ya serikali na mimi nimewaeleza hasa kwa dini ya Kiislamu ukimwona Muislamu siku ya kwanza hajachukua maiti yake na siku ya pili maana yake huyo mtu hana uwezo," alisema.

Waziri Ummy aliagiza waganga wafawidhi wa hospitali zote za serikali nchini kuzingatia miongozo ya kutozuia maiti na watafute njia zingine za kuruhusu maiti, waende kuzika, watakapomaliza watakwenda kudaiana mambo mengine.

Makonda alisema majibu hayo yamempa faraja kwa kuwa chama kinachoomba kura kinaona tatizo kinapomwona mtu ameshindwa kulipia mwili wa ndugu yake ambaye alimpeleka hospitalini kwa ajili ya kuokoa maisha yake.

Alisema kuna wakati mwingine mtu anauza kiwanja, wameweka rehani bidhaa zao na biashara zao kufilisika kuwatibu ndugu zao, hivyo kauli hiyo ya serikali ni faraja kwa wananchi.

"Kwa kuwa mimi ni msemaji, nitahakikisha hakuna mwananchi atakayeteseka. Ukishafiwa, kwanza ni pigo, wengine wanafiwa na baba zao, mama ama mtoto hawezi kuwapata tena, tunaishukuru serikali," alisema.

Waziri Ummy pia alisema kumejitokeza baadhi ya watumishi wa afya kutozingatia maelekezo ya maadili na miongozo mbalimbali katika kutoa huduma za afya.

"Kitu ulichokifanya Tanga ninakushukuru ningekuomba ukifanye nchi nzima kwa sababu tunataka kuhakikisha watendaji wa wilaya na mikoa wanawajibika kwa utoaji huduma za afya katika maeneo yao," alisema waziri.

Alisema kauli yake ni watumishi wa afya wanaokwenda kinyume cha miongozo na maelekezo ya serikali wachukuliwe hatua mara moja na viongozi wa mikoa na wilaya pale ambapo watabainika kufanya uzembe.

## Watumishi TEA watakiwa kutafuta rasilimali nchini

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), wametakiwa kuweka kipaumbele kwenye kutafuta rasilimali kwa ajili ya kusaidia shule mbalimbali nchini.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Dk. Erasmus Kipesha, alipozungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa mamlaka hiyo katika kikao cha pili cha baraza hilo.

Alisema ili TEA ifikie malengo hasa ya kutekeleza miradi kwa ufanisi kwenye shule mbalimbali nchini, ni lazima utafutaji rasilimali upewe kipaumbele na kila mtumishi wa mamlaka hiyo.

Dk. Kipesha aliipongeza Sekretarieti ya Baraza kwa maandalizi mazuri ya kikao hicho ambacho ni muhimu kwa ajili ya kupitia na kujadili masuala mbalimbali ya kiutumishi na utekelezaji majukumu ya mamlaka.

"TEA ilianzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Elimu na jukumu kuu la mfuko huo ni kutafuta rasilimali fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa masuala ya elimu ili kufadhili ujenzi wa miundombinu ya elimu, hivyo ninaomba kila mtumishi wa mamlaka aone anawajibika kutafuta rasilimali. "Tusidhani utekelezaji jukumu hili ni la mtu mmoja au idara moja ndani ya mamlaka. Huu ni wajibu wa kila mtumishi kutafuta vyanzo mbalimbali vya mapato ili tufikie malengo yetu kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema TEA ina wajibu wa kuhakikisha inakarabati na kujenga miundombinu ya shule mbalimbali nchini kama sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika utoaji elimu bora.

Alisema shule nyingi nchini zinahitaji huduma mbalimbali kutoka kwa mamlaka hiyo ikiwamo kujengewa vyoo bora, kuongezwa madarasa na madawati ili wanafunzi wasiketi sakafuni.

Alisema wanafunzi wanaposoma kwenye mazingira mazuri, wanakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufanya vizuri kwenye mitihani yao kulinganisha na wanapokuwa kwenye mazingira magumu ya kusomea.

TEA tangu kuanzishwa kwake imekuwa inakarabaati shule kongwe nchini, kujenga vyoo vya kisasa kwenye shule mbalimbali, kujenga visima vya maji na kuongeza idadi ya madarasa.

TEA pia inaendesha Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) ambao umewezesha zaidi ya vijana 48,000 mpaka sasa kupata ujuzi mbalimbali uliowasaidia kujiajiri na kuajiri wenzao kwenye ufundi mbalimbali.



**HABARI KASKAZINI**

# RC amaliza mgogoro wafugaji, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MGOGORO kati ya wafugaji wa jamii ya Kimasai wanaoishi katika Kijiji cha Kimotorok Wilaya ya Simanjiro na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, umemalizika baada ya serikali kuwakutanisha na kuweka makubaliano ya pamoja.

Wafugaji hao waliokuwa wakitishia usalama wa wahifadhi na askari wa hifadhi ulitokana na hasira yao ya kuzuiwa kuingiza mifugo yao ndani ya hifadhi kwa ajili ya malisho.

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alitangaza kumaliza mgogoro huo, baada ya menejimenti ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, kuiachia mifugo zaidi ya 800.

Akizungumza ya baada ya kurejesha mifugo hiyo kwa wafugaji, aliagiza viongozi wa kata na vijiji vinavyoizunguka hifadhi hiyo, kusimamia makubaliano na maelekezo ambayo yamepitishwa na serikali.

"Kila vikao vikifanyika mnapaswa kuwaambia wananchi ukweli pasipo kuwaficha, ili wapate uelewa juu ya maamuzi na maelekezo mbalimbali yanayotolewa, ili kuepusha migogoro isiyo na tija, " alisema Sendiga.

Alitoa maelekezo kwa menejimenti ya Hifadhi ya Tarangire, kuwaacha wafugaji waendelee kupata huduma za mifugo yao, ambayo bado inapatikana katika hifadhi, kama vile sehemu za kunyweshea mifugo.

Pia aliwataka wananchi hao kuendelea kutii sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa na kwa upande wa wahifadhi wajizatiti zaidi katika utoaji wa elimu na kuboresha mahusiano kati yao na wafugaji.

Diwani wa Loiborsiret, Ezekiel Lesenga (Mardadi), alimshukuru Queen Sendiga kwa kufanikisha urejeshwaji wa mifugo yao.

Lesenga alisema wafugaji sita wa Kijiji cha Kimotorok walikamatwa na ng'ombe160, mbuzi 260 na kondoo 340 wakashikiliwa.

Alisema askari wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire wamekamata mifugo hiyo ili hali haikuwa inachungiwa ndani ya hifadhi hiyo.

Mkazi wa Kata ya Loiborsiret, Dk. Frank Oleleshwa, alisema mgogoro wa mara kwa mara dhidi ya hifadhi hiyo na wananchi ilikaribia kupata muafaka wa kudumu, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuunda kamati ya mawaziri nane wa kisekta.

Oleleshwa alisema mawaziri hao ambao walifika hadi Kimotorok ili wamshauri Rais anaamini kamati ilishamaliza kazi yake kinachosubiriwa hadi sasa ni utekelezaji wa mapendekezo yao, ila hafahamu kinachokwamisha.

"Ninachoweza kushauri kwa sasa waliokaribu na Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, wamshauri juu ya kumuuliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, swali la moja kwa moja kwa nini taarifa ya kamati hiyo, haijawekwa hadharani kwa umma na kwanini hakuna hatua hazilizochukuliwa hadi leo?" alihoji.



Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Kaskazini, Cosmas Sadat, akipanda mti kati ya miti 500 iliyotolewa kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania, uliofanyika Kijiji cha Nakweni, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA GIFT THADEY**

# Serikali yaagiza minara ya simu 32 kujengwa Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG'

HATIMAYE serikali imeanza kurejesha mawasiliano ya uhakika ya mitandao ya simu katika Mkoa wa Manyara, baada ya kuagiza wawekezaji wa biashara hiyo kupeleka na kujenga minara mipya 32 ili kuongeza nguvu kutokana na iliyoko kuzidiwa.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza na Nipashe baada ya kutembelea eneo la Gendabi, Wilaya ya Hanang', alisema minara hiyo kwa sasa iko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Aidha alisema pia minara 388 itaongezewa nguvu iliyokuwa na uhafifu ili kuimarisha mawasiliano kwa wananchi.

Maafa hayo yaliyotokea Desemba 3, mwaka 2023, yalisababisha vifo vya watu 89 na kujeruhi vibaya wengine 139 katika Mji wa Katesh, vijiji vya Jorodom, Ganana, Katesh, Dumbeta, Gendabi, Sarijandu, Arukushay na Sebasi.

Jumla ya kaya 207 zilizokuwa na wakazi 322, zimepoteza makazi katika maeneo hayo.

Akiwa Hanang' Nape alisema lengo la ziara yake ni kuona maeneo yaliyoathirika na kutoa pole kwa wananchi na kuwashukuru wanahabari kwa kazi nzuri waliyofanya.

Lingine ni kuona maeneo itakapojengwa miundombinu ya taasisi zake kwenye makazi mapya ya wananchi waliokumbwa na maafa.

Pamoja na mambo mengine, alisema katika Mkoa wa Manyara, bado kuna shida ya mawasiliano kwa kuwa kuna milima mikubwa hasa vijijini ambayo inaathiri minara kuwa na ufanisi.

Waziri huyo alisema ili kutatua tatizo hilo, serikali ilishaelekeza kujengwa minara 758 nchi nzima ili kuondoa shida ya mawasiliano.

# Waliovamia Msitu wa Ketumbeine waanza kuondoka

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

ASILIMIA 50 ya wananchi wanaoishi katika vijiji vitatu vya Kata ya Ilorienito, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, waliokuwa wakidaiwa kuvamia Msitu wa Hifadhi wa Mlima Ketumbeine, wamehama rasmi eneo hilo.

Serikali ilitangaza ilani ya kuwataka kuondoka kwa lazima hadi kufikia kufikia Desemba 31, mwaka jana.

Diwani wa Kata ya Ilorienito, Sano Otusu, alisema hadi kufikia sasa wavamizi katika eneo hilo tayari wameondoka ili kutii bila shuruti amri ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Marko Ng'umbi.

Mwanzoni mwa Desemba, 2023, Mkuu wa Wilaya huyo, Marko Ng'umbi, alitoa nyongeza ya siku 18 ya kuwataka wananchi wa vijiji vya Nadare, Losirwa na Ilorienito waliovamia msitu huo kuondoka kwa hiari, badala ya kusubiri matumizi ya nguvu.

Wananchi hao ambao ni wafugaji wa jamii ya kimasai, wanadaiwa kuharibu vyanzo vya maji na kuhujumu shughuli za uhifadhi wa msitu huo kwa kuendesha shughuli za kilimo, kujenga makazi, kukata miti ovyo na kuchungia mifugo ndani ya vyanzo vya maji.

Kwa sasa mkakati wa kurejesha bioanuai katika mlima huo imeachwa mikononi mwa Shirika la Kimataifa la World Wide Fund (WWF), ambalo linaendelea na kampeni yake ya kurejesha uoto wa asili katika msitu huo wa hifadhi kwa kupanda miti.

Aidha alitoa miezi mitatu maboma yote yaliyojengwa ndani ya msitu huo wa hifadhi yawe yameondoka.


Kabla ya kuamuru waondoke wenyewe badala ya kusubiri matumizi ya nguvu, Mkuu huyo wa Wilaya, alikutana na kufanya mazungumzo na wananchi hao katika Kijiji cha Losirwa, Ilorienito, Nadale, Njoro Sokoni na Langa'ta Dabashi.

Alipoulizwa kuhusu mkakati huo, Meneja wa Mradi wa Land for Life, ulioko chini ya Shirika la Kimataifa la World Wide Fund (WWF), Reguli Marandu, alisema:

"Tumekuwa tukifanya kazi za uhifadhi katika vijiji vyenu na tukisema uhifadhi tunaangalia uhifadhi wa mazingira, tunaangalia uhifadhi wa wanyamapori lakini tunaangalia namna gani uhifadhi, unasaidia jamii zile zinazozunguka hayo mazingira, ambayo tunayahifadhi.

...Dhana ya WWF, tunataka jamii zile zinazoishi kwenye hayo mazingira pamoja na wanyamapori na mazingira yetu, vyote viwe vina ustawi ambao ni mzuri."

Msitu wa Hifadhi wa Ketumbeine ulitangazwa kuwa eneo la Msitu wa Hifadhi ya Mlima Ketumbeine mwaka 1958.



## W'biashara samaki Kamanga kupisha ujenzi wa bandari

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Aron Kalugumjuli, amesema tayari halmashauri hiyo imetenga eneo la Nella ikiwamo kuimarisha miundombinu kwa ajili ya kuwahamishia wafanyabiashara wanaopisha upanuzi wa Bandari ya Mwanza Kaskazini.

Amri ya kuhamishwa kwa wafanyabiashara hao wa dagaa na samaki katika eneo la Kamanga, ilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla baada ya kufanya ukaguzi wa mradi huo.

Makalla aliagiza kuongezwa kwa kasi ya upanuzi wa Bandari hiyo na kutaka kazi ya ujenzi ifanyike usiku na mchana ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

Aidha aliitaka Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuwahamishia wafanyabiashara hao kwenye eneo lingine ili wapishe ujenzi huo kwa maslahi mapana ya taifa.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Kanda za Ziwa Victoria, Erasto Lugenge, alisema maboresho pamoja na upanuzi wa bandari hiyo yanagharimu Sh. bilioni 18.6.

Alisema mradi huu ni miongoni mwa miradi mikubwa mitatu inayoendeshwa na serikali kupitia TPA na utekelezaji wake upo katika mkataba wa miezi 18 na unatarajia kukamilika Novemba mwaka huu.

Alisema mradi huo unavipengele 11 vinavyotakiwa kufanyiwa kazi ikiwamo upanuzi na uboreshaji wa gati kwa ajili ya kuegesha meli, ujenzi wa jengo la kusubiria abiria, jengo la ukaguzi wa abiria, uzio na kusakafia maeneo yote ambayo yanaizunguka bandari hiyo.

## Makamba asisitiza ushirikiano mawaziri Afrika Mashariki

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, amewasisitiza mawaziri wenzake wa Afrika Mashariki kutumia nyenzo za kawaida za kidiplomasia kukuza ushirikiano baina ya mataifa yao.

Alizitaja nyenzo hizo kuwa ni pamoja na midahalo ya kisiasa, Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPCs), mikutano ya majukwaa ya kiuchumi, Tume za Pamoja za Mawaziri (JMCs) na ziara za viongozi wa kitaifa. January alitoa msisitizo huo, jana jijini Kampala, Uganda muda mfupi baada ya kushiriki mkutano wa wakuu wa nchi na serikali wa nchi zisizofungamana na upande wowote na mkutano wa kundi la nchi 77+China. Alisema endapo vyombo hivyo vikitumika ipasavyo vitatoa fursa kwa pande husika kukuza biashara, uwekezaji, utalii pamoja na kutatua changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa masuala ambayo pande husika zimekubaliana.

"Katika mkutano huu nimekutana na mawaziri wa mambo ya nje wanaotoka katika nchi mbalimbali ikiwamo Kenya, Msumbiji, Somalia, Malawi, Misri, Ghana, Morocco, Filipino, Ethiopia, Singapore, Vietnam, Cuba, Iraq, Bahamas, Venezuela, Jamhuri ya Kidemokrsia ya Congo(DRC) na Azerbaijan.

"Nimeshiriki kwa muda wa siku tatu katika mikutano hiyo na nimekutana na mawaziri 17 kutoka nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na nchi hizo na kuweka mikakati ya kushirikiana kiuchumi kwa manufaa ya pande zote," alisema January huku akisistiza kwa akauli yake ya 'vitu lazima vitokee.'

Mkutano huo, umekusanya takriban theluthi mbili ya nchi zote duniani kama fursa muhimu ya kuitangaza Tanzania kidiplomasia na kujadili mikakati na nyenzo za kujiletea maendeleo na kutatua changamoto zinazoikabili dunia.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati), akikata utepe kuashiria kuzinduliwa kwa jengo la abiria la Kiwanja cha Ndege Wilaya ya Kahama kilichojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 896.7, kushoto kwake ni Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mboni Mhita na viongozi wengine jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wagoma kuripoti shuleni kisa wahitimu kukosa ajira

**Na Waandishi Wetu**

ZIKIWA zimepita wiki mbili tangu shule zifunguliwe nchini baadhi ya wanafunzi waliotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza katika maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa, wamegoma kuripoti kwa kigezo kuwa wenzao waliomaliza wapo mitaani bila kupata ajira.

Wamesema kuwaona wenzao waliohitimu kidato cha nne, sita na chuo kikuu kuwapo mitaani bila ajira wala shughuli maalumu kumewakatisha tamaa ya kujiunga na masomo ya sekondari na kuamua kutafuta shughuli nyingine zitakazowainua kiuchumi ukiwamo ufundi.

Nipashe ilimtafuta mmoja wa wazazi wa watoto ambao hawajaripoti shuleni licha ya kufaulu vizuri, Elizabeth Charles ambaye ni Mkazi wa Mtaa wa Mkuyuni, Kata ya Turwa wilayani Tarime mkoani Mara ambaye alisema binti yake alikataa kabisa kuandikishwa na kutaka apelekwe chuo cha ufundi.

"Ni kweli binti yangu amefaulu vizuri na amepangwa katika Shule ya Sekondari Tuwa lakini amegoma kabisa kwenda kuripoti badala yake ameomba akasomee ufundi chereani na hii ni kutokana na idadi kubwa ya wahitimu kuwa mitaani bila kazi maalum," alisema Elizabeth.

Baadhi ya wazazi ambao bado hawajapeleka watoto wao shule, walisema wanaendelea kujipanga kuwatimizia mahitaji watoto wao ikiwamo kuwanunua vifaa vya shule, wakieleza kwamba mtoto akienda shule bila sare atajisikia mnyonge kwa kuona wenzake wamevaa sare.

Mpaka kufikia jana Mkoa wa Mara ulikuwa umesajili wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa asilimia 61, darasa la kwanza asilimia 90.3, awali ni asilimia 78.7.

Katika Mkoa wa Shinyanga waliosajiliwa kujiunga na kidato cha kwanza ni asilimia 50, darasa la kwanza asilimia 81 na awali asilimia 70, vilevile katika Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza waliosajiliwa kwa kidato cha kwanza ni asilimia 32.63, la kwanza 75% na awali 44%.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, aliiambia Nipashe kuwa wanafunzi 107,007 wameripoti mkoani humo kufikia Januari 17, 2024 ambapo ni pamoja na wale wa elimu ya watu wazima.

"Matarajio ilikuwa ni kuandikisha wanafunzi wa awali 82,679, lakini hadi sasa wameandikishwa 6576, darasa la kwanza wanafunzi 74,234.

Alisema wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ni 52,784, walioripoti ni 32,212, ambapo wanafunzi wa elimu ya watu wazima ni 503," alisema.

Ofisa Elimu wa elimu ya watu wazima mkoani Shinyanga, Dedan Rutazika, akizungumza na Nipashe kwa niaba ya Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako alisema: "Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, matokeo ya wanafunzi wa awali kuandikisha ni 75,079, wavulana 37,517, wasichana 37,562, lakini hadi sasa tumeandikisha wanafunzi 52,555, wavulana 26,262, wasichana 26,293 sawa na asilimia 70".

Alisema kwa darasa la kwanza matokeo yalikuwa ni kuandikisha wanafunzi 69,792, wavulana 34,641, wasichana 35,151, hadi sasa wameandikisha wanafunzi 56,452, wavulana 27,898, wasichana 28,554 sawa na asilimia 81.

Kuhusu wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wameripoti shule hadi sasa, alitaja waliochanguliwa kuwa ni 38,570, wavulana 21,853, wasichana 16,717, ambao wameanza masomo ni 19,307, wavulana 8,385, wasichana 10,922 sawa na asilimia 50.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Prof. Siza Tumbo, aliwataka wazazi kuwapeleka watoto wao kuanza masomo hata kama hawana sare za shule.

Ziara iliyofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Paulo Chacha, kwa zaidi ya shule 30 wilayani humo imetajwa kubaini idadi kubwa ya watoto kutoripoti shuleni, huku baadhi yao wakipelekwa kufanya kazi za ndani, kwenye madini, kuolewa, kuchunga mifugo na uvuvi.

Aliiambia Nipashe kuwa ameanza ziara ya nyumba kwa nyumba kwa wazazi walioshindwa kupeleka watoto wao shuleni tangu zilipofunguliwa kwa mwaka mpya wa masomo.

Aidha, aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama wilayani humo kushughulika na wazazi hao mara moja na kuhakikisha wanawapeleka wanafunzi shule kupata haki yao ya msingi.

Hivyo, aliwataka watendaji wote wa kata na vijiji vyote 115 wilayani humo kuwafuatilia wazazi waliowaficha watoto kutoripoti shule pamoja na wanafunzi wanaofanya kazi sehemu mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, aliwataka wazazi wilayani humo kuhakikisha watoto wanapelekwa shule kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwalinda dhidi ya vitendo vya kikatili.

Kadhalika alipiga marufuku watoto wenye umri wa kuanza shule kuonekana wakizurura mitaani hususani katika muda wa masomo, huku akiwataka wale ambao hawajajiunga na kidato cha kwanza kufanya hivyo haraka.

**-Imeandaliwa na Timothy Itembe (MARA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Shaban Njia (KAHAMA), Vitus Audax (MWANZA)**

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 11 WENYE 'ASSIST' NYINGI LIGI KUU 14



Wachezaji wa Ivory Coast wakishangilia baada ya kupata bao la kwanza dhidi ya Guinea Bissau kwenye mechi ya ufunguzi ya Afcon nchini humo wakati wakishinda 2-0 Januari 13, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# AFCON ILIVYOZIKA MACHUNGU YA VITA NCHINI IVORY COAST

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KWA mujibu wa serikali ya Ivory Coast dola bilioni moja zimetumika kuandaa mashindano ya Mataifa ya Africa, Afcon, yanayoendelea nchini humo baada ya kujenga viwanja vinne vipya na kukarabati vingine viwili.

Aidha, viwanja vya ndege, barabara, hospitali na hoteli zimejengwa au kuboreshwa katika miji mitano inayoandaa mechi; Abidjan, Bouake, Korhogo, San Pedro na Yamoussoukro.

Ni ujenzi mkubwa wa maendeleo katika taifa hilo la Afrika Magharibi tangu vita vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 2002 hadi 2007 na 2010 hadi 2011. Baadhi ya fedha za ujenzi zimetokana na mkopo wa dola za Kimarekani bilioni 3.5 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Aprili mwaka jana.

Huku Ivory Coast ikiorodheshwa kama taifa la 138 kati ya 190 na IMF kwa ukubwa wa uchumi. Uchumi wake umekua kwa wastani wa asilimia nane kwa mwaka tangu Rais Alassane Ouattara, mfanyakazi wa zamani wa IMF achukue madaraka 2010.

"Ivory Coast ni nchi maskini," Prao Yao Seraphin, profesa wa uchumi wa Ivory Coast, anaiambia BBC Sport Africa.

"Kutokana na hali hiyo, Rais Ouattara amelazimika kuchukua mikopo kufadhili mradi huu, hivyo tunapaswa kuhakikisha mikopo hiyo inanufaisha Ivory Coast. Nchi italazimika kutunza miundombinu."

Ivory Coast, ambayo wakati mmoja ilikuwa nyumbani kwa mojawapo ya idadi kubwa zaidi ya tembo barani Afrika - ndio mwenyeji wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka huu.

**Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny**

Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, ulioandaa mechi za ufunguzi na fainali ya Kombe la Mataifa ya mwaka 1984, umekarabatiwa kwa ajili ya fainali ya mwaka huu.

Baada ya kutumia zaidi ya dola bilioni 1 - huku baadhi ya ripoti za vyombo vya habari zikiripoti mara mbili ya kiasi hicho kama ya maandilizi - Ivory Coast inasema haijandaa mashindano hayo ili kupata fedha.

Francois Amichia, anaendesha kamati ya maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Afrika, anasema "Ivory Coast ilipoamua kuandaa kombe hili, haikuwa kutafuta fedha bali kujipanga upya," anasema Amichia, ambaye pia ni mbunge na waziri wa zamani wa michezo.

"Ni fursa kujenga miundombinu ya michezo na lazima niwakumbushe hakuna miundombinu ya michezo iliyojengwa kwa miaka mingi - Kombe la Mataifa ya Afrika limeruhusu kuwa na viwanja vinne vipya na viwili vilivyokarabatiwa."

Kiasi cha dola za kimarekani milioni 79, milioni 84 na milioni 113 zimetumika kujenga viwanja vipya Yamoussoukro, Korhogo na Abidjan huku ukarabati wa Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, Abidjan ukigharimu dola za Kimarekani milioni 109.

Uwanja huo ulijengwa mwaka 1964, baadaye nchi hiyo ikawa mwenyeji Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 1984, na Uwanja wa Bouake ulijengwa kwa fainali hizo.

Vituo 24 vya mazoezi vimejengwa au kukarabatiwa katika miji mitano. Jengo moja moja la kifahari la vyumba 32 limejengwa Bouake, San Pedro na Yamoussoukro na hoteli ya vyumba 48 huko Korhogo.

Hospitali za Korhogo na San Pedro zimeboreshwa na viwanja viwili vya ndege - pia vimefanyiwa ukarabati. Barabara kuu kutoka Abidjan - zote mbili za magharibi hadi pwani ya San Pedro, na kaskazini hadi Korhogo zimekarabatiwa.

"Tunajua Ivory Coast ilipitia kipindi kigumu, ambacho hakikuwa rahisi kiuchumi. Lakini Kombe hili limeruhusu Ivory Coast kujitayarisha na miundombinu ya kimichezo na isiyo ya kimichezo," anasema Amichia.

Shirikisho la Soka la Ivory Coast (FIF), limekuwa likipanga jinsi ya kushughulikia wasiwasi wa kama Profesa Seraphin juu ya mustakabali wa viwanja vipya na gharama.

Waliandaa Ligi ya Mabingwa ya Afrika kwa Wanawake Novemba. Raia wa Ivory Coast wanataka kuwa kituo cha uandaaji wa michezo kikanda - hasa kwa kuwa nchi jirani viwanja vyao vya kitaifa havikidhi vigezo vya kuandaa michezo ya kimataifa.

"Tutahakikisha nchi yetu inakuwa kitovu cha Afrika Magharibi katika masuala ya soka na mashindano ya michezo," anasema rais wa FIF, Idriss Diallo.

"Tutatoa nafasi kwa nchi zote ambazo hazina miundombinu iliyoidhinishwa na Shirikisho la Soka Afrika na Fifa."

Rais Ouattara ana nia ya kuhakikisha ukanda huo una miundombinu bora ya michezo - kupitia mradi wa pamoja na Ufaransa wa kujenga viwanja 10 vidogo vya michezo kote Ivory Coast.

**Fursa nzuri kwa biashara**

Hospitali mpya imejengwa Bouake, Ivory Coast kwa ajili ya michuano hii.

Tangu kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe - zaidi ya watu milioni moja walikimbia makazi yao, Ivory Coast imepanda kiuchumi.

Profesa Seraphin wa Chuo Kikuu cha Alassane Ouattara huko Bouake, anaamini manufaa ya Kombe la Mataifa yatakuwa ya muda mfupi na muda mrefu.

"Faida ya kwanza ya muda mfupi itaongeza mvuto wa Ivory Coast kwa wawekezaji binafsi, kwani macho ya dunia yatakuwa kwetu."

"Pia kutakuwa na biashara nyingi, ajira zitatolewa katika hoteli tunapokaribisha wageni na utalii ambao unawakilisha karibu asilimia tisa ya pato la Taifa."

Seraphin anaamini viwanja vilivyoboreshwa vitawapa raia wa Ivory Coast shauku mpya ya kuhudhuria michezoni, haswa kwa kuwa na migahawa na biashara.

"Watu wa Korhogo, Bouake, Yamoussoukro na San Pedro watafaidika na viwanja hivi pamoja na hospitali na vituo vya afya vilivyoboreshwa - na nchi itafaidika na ukarabati huu mkubwa."

## ISIKUPITE

SENEGAL itaongoza Kundi C ikiwa itaepuka kushindwa katika mechi yao ya mwisho dhidi ya Guinea kesho. Aliou Cisse aliwaongoza 'Simba wa Teranga' hao kutwaa taji lao la kwanza la Afcon miaka miwili iliyopita, na sasa wameanza vema mbio za kutetea ubingwa wao, wakitaka kuwa timu ya kwanza kubeba kombe hilo mara mbili mfululizo tangu 2010 wakati Misri ilipo-shinda kwa mara ya tatu mfululizo.



## Extra Time



Wachezaji wa Senegal wakishangilia moja kati ya mabao 3-0 waliyofunga dhidi ya Gambia kwenye michuano ya Afcon inayoendelea nchini Ivory Coast. **PICHA: MTANDAO**

# JINSI SENEGAL ILIVYOKUJA KUTAWALA SOKA LA AFRIKA

**ABIDJAN, Ivory Coast**

HUENDA Morocco iliweka historia mwaka 2022 kwa kuwa timu ya kwanza ya Afrika kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia, lakini kikosi kikuu cha soka barani humu kipo chini zaidi ufukweni mwa Senegal.

Simba wa Teranga wanatetea ubingwa wake wa Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Ivory Coast mwezi huu na tayari wamefuzu hatua ya 16-bora.

Senegal pia wanatawala mabingwa wa bara katika ngazi ya umri chini ya miaka 17 na chini ya umri wa miaka 20, na hata kushinda ubingwa wa Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) kwa mara ya kwanza mwaka jana.

Vijana hao wa Kocha Aliou Cisse walianza kampeni yao ya Kundi C kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Gambia Jumatatu iliyopita wakiwa wanamulika kuwa timu ya kwanza kusajili ubingwa mfululizo wa Afcon tangu Misri iliposhinda mara tatu mfululizo mwaka 2010.

"Tuna nyota moja tu," anasema Cisse mwenye umri wa miaka 47, akimaanisha kuwa alinyanyua kombe mara moja tu.

"Tuna nia ya kushinda tena, ili kuendelea kushinda."

Cisse mwenyewe alikuwa sehemu ya kizazi cha dhahabu cha Senegal, ambacho kilimaliza kama washindi wa pili kwenye Afcon ya 2002 kabla ya kufika robo fainali ya Kombe la Dunia baadaye mwaka huo katika michuano ambayo nchi hiyo ilikuwa ikishiriki kwa mara ya kwanza.

Mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya taifa, El Hadji Diouf anaamini mafanikio ya hivi karibuni ya Senegal ni matokeo ya ushirikiano mkubwa kati ya serikali na shirikisho la soka nchini humo (FSF) na uwekezaji muhimu katika vituo vya kulelea vipaji.

"Kila mahali unapoenda Senegal, miji yote ina akademi," anasema Diouf akiiambia BBC Sport Africa.

"Wanaanza wachanga, chini ya umri wa miaka 10, na wana mashindano kila mwaka. Tunataka kuboresha hilo na kuwa sawa na Uingereza na Ufaransa.

"Napenda kusema hongera na shukrani kwa serikali kwa sababu ya sera na wanatoa fedha. Na rais wa FSF, Augustin Senghor, anafanya kazi vizuri sana."

Senegal pia inashikilia ubingwa wa soka la ufukweni, huku nchi hiyo ikishinda mataji manne ya bara na kumaliza nafasi ya nne kwenye Kombe la Dunia la Soka la Ufukweni nchini Urusi mwaka 2021.

### Njia na uthabiti wa kufundisha

Cisse alikuwa nahodha wa Senegal katika Kombe la Mataifa ya Afrika na Kombe la Dunia mwaka 2002, na amekuwa kocha wa timu ya taifa tangu mwaka 2015.

Licha ya uanzishwaji wa shule za mitaa na miundombinu, Souleymane Diallo, mkufunzi wa muda wa makundi ya umri wa kitaifa na profesa wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Cheikh Anta Diop huko Dakar, anasema njia imeundwa ili kuhamisha vipaji kutoka ngazi ya kimataifa ya vijana hadi ya juu.

"Senegal ina uwezo wa ajabu wa wachezaji na tunavivumilia vizazi," anasema Diallo akiiambia BBC Sport Africa.

"Katika ngazi ya chini, tuna msingi mpana sana na tunatengeneza njia ambazo wachezaji hawa wanaweza kufikia kikosi cha kwanza.

"Shirikisho linaomba tuwaweke kwenye rada wachezaji waliocheza katika viwango vya chini ili kila kizazi kiweze kutoka ngazi ya chini kwenda juu zaidi.

"Ikiwa watamaliza kategoria yao wakiwa U-17, wataenda U-20. Wakimaliza U-20 wanakwenda U-23, timu ya CHAN na timu ya kwanza."

Sababu nyingine kubwa katika mkakati wa muda mrefu wa Senegal imekuwa ni kuhakikisha uthabiti.

Cisse amekuwa akiwaongoza Simba wa Teranga tangu Machi 2015, na polepole amejijenga kuelekea mafanikio.

Kutolewa kwenye robo fainali katika Afcon 2017 (kwa mikwaju ya penalti) kulifuatiwa na kushindwa katika fainali ya 2019, kabla ya Senegal kurejea Cameroon Februari 2022.

Wakati huo Waafrika Magharibi hao walikuwa timu iliyoorodheshwa kuwa bora zaidi kwa bara la Afrika kwa zaidi ya miaka minne kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Morocco kutokana na mbio zao za kihistoria za Kombe la Dunia.

Mashabiki wa Senegal wamezoea kutazama timu kutoka nchi hiyo ikinyakua mataji ya bara, lakini wameshuhudia kutolewa mapema kwenye Kombe la Dunia la 2022.

Senegal ilitoka katika hatua ya 16 bora nchini Qatar, kwa kuchapwa mabao 3-0 na England, lakini hakukuwa na maswali juu ya mustakabali wa Cisse.

"Sera ya Senegal ni kusisitiza kwamba makocha wanabaki kwenye benchi la timu ya taifa kwa muda mrefu iwezekanavyo," anasema Diallo.

"Mchoro umewekwa ambao unahakikisha makocha wote wa kitaifa wana mahitaji sawa katika suala la maudhui ya mafunzo na habari, na kuunda njia za mawasiliano."

Kushiriki katika mashindano ya bara na kimataifa katika ngazi ya vijana mara kwa mara kumesaidia kukuza ustawi wa taifa.

"Mchakato wa kufikia ngazi ya juu ni wa taratibu," anasema Diallo.

"Hapo awali, hatukushinda Afrika kwa sababu hatukushiriki mara kwa mara katika mashindano ya Afrika.

"Kama unataka kushinda lazima uwapo kwanza, hatua ya kwanza ni kutatua tatizo la kuwapo kwenye mashindano haya, na ndicho ambacho Senegal wamefanya.

"Tunahitaji kuwapo wakati wote, na ni sasa kwamba tutaweka misingi ya kushinda Kombe la Dunia katika siku zijazo."

### Hakuna cha kuogopa nchini Ivory Coast

Kuhusu utetezi wao wa ubingwa wa Afcon, wasiwasi umeibuka kuhusu ukweli kwamba baadhi ya wachezaji muhimu wa Senegal sasa wanacheza nchini Saudi Arabia, huku kipa Edouard Mendy, nahodha Kalidou Koulibaly na 'hirizi' yao, Sadio Mane, wote wakiwa huko.

Hapo awali Cisse alikataa kuchagua wachezaji kutoka Saudi Pro League kwa sababu ya ubora wake wa chini ukilinganisha na wale wanaocheza Ulaya. "Tulionesha tulikuwa na uwezo wa kushinda taji tulipokuwa na wachezaji katika michuano mikubwa ya Ulaya," anasema Cisse.

"Sasa lazima pia tuoneshe tunaweza kushinda tukiwa na wachezaji wanaocheza Saudi Arabia."

Diouf ana wasiwasi kuhusu nafasi ya Senegal ya kutetea kombe hilo, na anasema fowadi wa zamani wa Liverpool na Bayern Munich, Mane "anataka kuonesha kila mtu."

"Sisi ni timu bora zaidi barani Afrika na hatupaswi kuogopa chochote," anasema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 42.

"Tuna ubora mwingi na naona wachezaji bado wana njaa, mchanganyiko tulionao kati ya viongozi wa timu hii na vijana ni mzuri zaidi.

"Njia pekee ambayo hatuwezi kushinda Kombe hili la Mataifa ya Afrika ni kwa kutofikiri sisi ni bora."

Na Mane, ambaye alifunga mkwaju wa penalti wa ushindi katika fainali dhidi ya Misri nchini Cameroon chini ya miaka miwili iliyopita, anajua hamasa itakavyokuwa wakirudisha kombe hilo.

"Kushinda Afcon lilikuwa kombe bora zaidi kuwahi kutwaa maishani mwangu na kuja kulifanya tena litakuwa jambo la kipekee na mafanikio makubwa zaidi," anasema akiiambia Caf Online.

"Kushinda Afcon kutakuwa na hamasa kubwa kwa soka letu kwa sababu tumeshinda makundi mengine yote, ambayo ni mazuri kwa nchi."

## Nukuu

"Ni kweli haiwezekani kwangu kwenda kwenye Ligi ya Saudia leo. Hakuna nafasi. Milioni 10, 20 au 30 hazitabadilisha maisha yangu. Niko Real Madrid, klabu bora zaidi duniani. Napenda maisha yangu Madrid, ndivyo hivyo kwa familia yangu, na ndivyo hivyo tu," **Kiungo wa kati wa Real Madrid, Fede Valverde, akieleza ni kwa nini amekataa ofa kutoka Saudi Arabia licha ya kuahidiwa kulipwa mshahara mnono.**



"Mechi hii ilikuwa muhimu sana kujenga kasi yetu tena. Kutolewa kwenye Kombe la FA iliniumiza sana kwa hivyo nina uhakika tutaitumia kutoa msukumo kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa mwezi ujao. Ukiangalia kwenye ligi unataka kuwa wa kwanza - si wa nne, au wa sita au wa tatu. Unataka kuwa wa kwanza," **Winga wa Arsenal, Bukayo Saka, baada ya juzi kuichapa Crystal Palace mabao 5-0 kwenye Ligi Kuu, akielezea hasira zao za kutolewa na Liverpool kwenye FA Cup.**



"Hiki ndicho nilichopenda kwake. Beki anafanya uamuzi mbaya... lakini ana utulivu, utulivu mbele ya goli. Huyo alikuwa Thierry Henry, akiingia katika maeneo hayo, alikuwa mzuri katika kufanya hivyo," **Beki wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand akimsifu na kumfananisha mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Martinelli na nguli wa zamani wa klabu hiyo, Thierry Henry. Martineli juzi alitokea benchi na kufunga mabao mawili wakati wakiipiga Crystal Palace 5-0.**



# WACHEZAJI 11 WENYE 'ASSIST' NYINGI LIGI KUU




Kinara wa 'assist' Ligi Kuu Bara, Kipre Junior.

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara iliposimama mwishoni mwa Desemba mwaka jana, takwimu ziliandikwa na wachezaji. Kuna wanaoongoza kwa kufunga mabao mengi kwa mguu wa kulia, kushoto, vichwa, penalti na faulo.

Mara nyingi watu wanaotoa usaidizi wa kufunga mabao husahauliwa. Lakini hawa ni muhimu sana kwenye mchezo wa soka kwa sababu wanatengeneza nafasi ili wenzao wafunge na kuleta raha ya mpira wa miguu.

Katika makala haya tutawangalia wachezaji 11 ambao wametoa pasi nyingi za mabao kwenye Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya 14 iliposimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi na fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazoendelea nchini Ivory Coast.

Ilikumbukwe pia msimu uliopita wa 2022/23 Clatous Chama wa Simba ndiye aliyeibuka kinara wa 'assist' akitoa pasi 14 zilizozaa mabao.

**11# Jacob Massawe (Namungo)- asisti 3**

Ni mmoja wa mastraika wakongwe kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Anakumbukwa tangu akiwa kwenye kikosi cha Stand United kilichokuwa kinacheza ligi na kuwa kwenye kilele cha ubora wake 2019.

Kwa sasa anaichezea Namungo FC, pamoja na kwamba hajafunga bao lolote mpaka sasa msimu huu, lakini ametoa pasi tatu za mwisho zilizosaidia timu yake kupata mabao.

**10# Djibril Sillah (Azam FC) - asisti 3**

Yupo kwenye kiwango bora Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa amesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu. Raia huyu wa Guinea ameshaifungia Azam FC mabao matatu, lakini ana 'asisti' tatu mpaka sasa.

**9# Luis Miquissone (Simba) - asisti 3**

Licha ya kwanza mpaka sasa hajapata namba ya kudumu katika Kikosi cha Simba, huku akiwa ndiyo kwanza anaonekana ameanza kurejea kwenye kiwango chake kilichozoeleka, lakini zile dakika chache alizopata amefanya kitu cha manufaa kwenye timu yake.

Ametoa pasi tatu za mwisho zilizozaa mabao kwa timu yake ya Simba, tena kipindi hicho akiwa bado hayupo fiti kabisa. Miquissone, raia wa Msumbuji amerejea tena Simba msimu huu, baada ya klabu hiyo kumuuza kwenda Al Ahly ya Misri mwaka 2021.

**8# Clament Mzize (Yanga) - asisti 3**

Ana bao moja tu alilolifunga katika mechi ambayo Yanga ilicheza dhidi ya Coastal Union, Novemba 8, mwaka jana, akiisaidia timu yake kushinda 1-0. Pamoja na hayo amekuwa na msaada ya kutoa pasi za mwisho kwa wenzake kwani mpaka sasa, Mzize ana asisti tatu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**7# Ladack Chasambi (Mtibwa) - asisti 3**

Ameondoka Mtibwa Sugar kipindi hiki cha uhamisho wa dirisha dogo na kujiunga na Klabu ya Simba. Winga huyu ameiachia klabu yake hiyo ya zamani asisti tatu, huku akienda kuanza tena maisha mapya. Kama kanuni zinavyosema hata akiwa kwenye timu yake mpya akifanya kama hivyo, asisti zitaendelea kuhesabika pale alipoishia.

**6# Lusajo Mwaikenda (Azam FC) - asisti 4**

Ni beki wa pembeni wa Azam FC ambaye mbali na kazi yake mama ya kuzuia, lakini mpaka sana ameisaidia timu yake kutoa pasi nne za mwisho za usaidizi wa mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**5# Impiri Mbombo (Tabora United) - asisti 4**

Raia huyu wa Kidemokrasi ya Congo, ni mmoja kati ya wachezaji wanaoifanya Tabora United iwe timu tishio kwa sasa kwenye Ligi Kuu. Ameitengenezea asisti nne mpaka sasa, ikiwa ni karibia ya nusu ya mabao yote ya timu hiyo. Tabora United imefunga mabao tisa mpaka sasa kwenye ligi hiyo ikiwa nafasi ya 12 na pointi 15.

**4# Awesu Awesu (KMC) - asisti 4**

KMC ina kiungo mshambuliaji wake anayeitwa Awesu Awesu. Msimu huu amerejea kwenye kiwango chake cha hali ya juu ambacho alikuwa nacho miaka ya nyuma akiwa Kagera Sugar. Ana bao moja kibindoni mpaka sasa, lakini ana asisti nne mpaka sasa, jumla akiwa amechangia mabao matano kati ya 15 ambayo timu yake imepata mpaka sasa.

**3# Feisal Salum (Azam FC) - asisti 4**

Yupo kwenye kiwango cha juu kuliko wakati mwingine wowote kwenye wasifu wake wa soka kitakwimu. Kiungo mshambuliaji huyo ametoa pasi za usaidizi nne zilizozaa mabao kwenye timu yake mpya ya Azam aliyojiunga nayo msimu huu akitokea Yanga, lakini pia kwenye kupachika mabao usiseme. Yupo kwenye nafasi ya tatu, akiwa amepachika mabao manane mpaka sasa kwenye ligi.

**2# Yao Kouassi (Yanga)- asisti 5**

Ndiye beki anayeongoza kwa kuwa na 'assist' nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Yanga ilimsajili beki huyu wa kulia kutoka Klabu ya Asec Mimosas ya Ivory Coast na amekuwa mhimili mkubwa kwa kikosi hicho.

Mbali na kazi yake ya kuzuia mawinga machachari, amekuwa akisaidia mashambulizi, mpaka sasa akiwa na 'assist' tano, akiwa pia amepachika bao moja mguuni mwake alilolifunga Agosti 29, mwaka jana, Yanga ikiifunga JKT Tanzania mabao 5-0, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

**1# Kipre Junior (Azam FC) - asisti 6**

Alisajiliwa 2022 akitokea kwenye Klabu ya Sol FC ya nchini mwao Ivory Coast. Alianza kwa kuuwasha moto kwenye klabu yake mpya, lakini kuna wakati alipotea. Kiwango kilionekana kuporomoka.

Msimu huu amekuwa kwenye kiwango bora kwani ametengeneza nafasi sita za kufunga, akiwa mchezaji anayeongoza kwa 'assist' nyingi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kiungo huyo mshambuliaji ambaye pia hucheza kama winga, amepachika mabao manne.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 5-0 juzi dhidi ya Arsenal, kinaifanya Crystal Palace sasa iwe imeshinda mechi moja tu kati ya 11 zilizopita za Ligi Kuu England na nafasi yao kwenye jedwali inazidi kuwa mbaya. Wako nafasi ya 14, pointi tano juu ya eneo la kushuka daraja, lakini wamecheza mchezo zaidi ya Luton iliyopo katika nafasi ya 18.



# Bashungwa: Ni aibu kwa karne hii Tanzania kuwa na barabara mbovu

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema ni aibu katika karne ya 21 Tanzania kuwa na barabara ambazo hazipitiki kipindi cha msimu wa mvua, hali ambayo inachangia baadhi ya shughuli za kiuchumi kusimama.

Bashungwa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhusu tatizo la maji kujaa juu ya Barabara ya Dodoma- Morogoro na kukata mawasiliano katika Kijiji cha Mtanana wilayani Kongwa.

"Ni aibu kwa taifa letu ambalo limeingia kwenye uchumi wa kati wa chini na karne hii ya 21 kuwa na barabara ambayo ndiyo nyenzo muhimu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kuwa hazipitiki eti tuu kwa sababu ya mvua."

"Haiwezekani magari yanasubiri mvua zikatike ndiyo yaendelee na safari watu wanasubiri hapa hadi nusu siku ndiyo wapite jambo hili halikubaliki na serikali hii ya Rais Samia," alisema Bashungwa.

Alisema kutokana na hali hiyo alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi kutumia wataalamu wake kubaini tatizo la maji kujaa juu ya barabara hiyo na kulitafutia suluhu ya kudumu.

"Baada ya hali hii kutokea nilimwagiza Katibu Mkuu kuhakikisha anatumia wataalamu wake kufanya tathmini ya eneo hili na kuja na suluhu ya muda mfupi na muda mrefu."

"Lakini katika suluhu ya muda mfupi mtakayoifanya hapa mhakikishe haiharibu suluhu ya muda mrefu siyo baadaye tena kuja hapa na hichi tulichokifanya kwa wakati huu kinakuwa hakina maana," alisema.

Kadhalika, aliagiza hadi ifikapo Desemba mwaka huu suluhu ya kudumu katika eneo hilo iwe imepatikana ili kuondoa tatizo la mawasiliano kukatika katika barabara hiyo muhimu kiuchumi. Vile vile, Bashungwa akiwa wilayani Mpwapwa kukagua ujenzi wa barabara ya kilomita 33 kwa kiwango cha lami ya Kongwa Mpwapwa alisema serikali haitawavumilia makandarasi wababaishaji.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu miradi ya barabara ambayo imekuwa ikijengwa chini ya kiwango.

"Niwaagize Bodi ya Usajili Makandarasi pamoja na Bodi ya Wahandisi kuhakikisha wanachukua hatua kali kwa yeyote ambaye atafanya mambo kinyume na maadili ya taaluma hiyo," alisema.

Naye Mbunge wa Mpwapwa, George Malima, aliishukuru serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami hali ambayo itasaidia kurahisisha mawasiliano hasa wakati wa masika.



Wakazi wa Kata ya Chamwino waliojitokeza kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo ya makaburi ya Hijra yaliyoko Chinangali Jiji la Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wafugaji, wawindaji waonywa kujichukulia sheria mkononi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida imewaonya wafugaji na wawindaji wa jamii ya Wahdazabe kuacha kujichukulia sheria mkononi katika kugombea mipaka ya ardhi na badala yake waache mamlaka husika zishughulikie suala hilo. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Asia Messos, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wananchi hao wa Kijiji cha Munguli, Kitongoji cha Kipamba Kata ya Mwangeza.

Hatua ya Mkurugenzi huyo kutoa onyo hilo inatokana na wafugaji kudaiwa kuharibu mizinga ya nyuki iliyotolewa na serikali kwa jamii ya Wahdazabe kujipatia kipato kupitia asali.

Messos alisema serikali imejipanga kushughulikia migogoro mbalimbali ukiwamo huo wa mpaka na hivyo hakuna sababu ya kujichukulia hatua mkononi.

"Kimsingi tumesikitishwa kuona jamii hizi zimekuwa na mgogoro na kufikia hatua ya kuharibu mizinga tunataka amani itawale mgogoro katika mgogoro huu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wananchi lazima watii mamlaka kwa kufuata sheria zilizopo ili kupata haki zao sambamba na kuacha tabia ya kulea wahalifu wanaosababisha migogoro katika jamii.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi huyo amewataka wananchi wa Kijiji cha Gumanga, Kata ya Gumanga kutumia mafunzo waliyoyapata ya namna ya kupata msaada wa sheria kwa ajili ya kujipatia haki katika masuala mbalimbali.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kuhitimisha siku 10 za Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia wilayani Mkalama ili kuhakikisha wananchi wanapatiwa ufumbuzi wa changamoto zao.

Naye Ofisa Ardhi Wilaya ya Mkalama, Protas Majumba, alisema kuna sheria ya ardhi ya jumla, vijiji na hifadhi huku akisisitiza kila ardhi inasheria yake, hivyo ni muhimu wananchi kutambua sheria hizo ili inapotekea changamoto wajue ni wapi wanaweza kupata haki zao.

# Wagonjwa wa kiharusi 1,531 wapokelewa BMH mwaka jana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH), kwa mwaka 2023 imepokea wagonjwa wa kiharusi 1,531 ambao walikwenda kupata matibabu.

Msemaji wa hospitali hiyo, Raymond Mbwambo, alitoa takwimu hizo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema wagonjwa hao ni wale ambao walifika kupata matibabu na kurudi nyumbani na wengine wanalazwa kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

"Tunaendelea kutoa matibabu kwa wagonjwa wa kiharusi hivyo msiwafiche wagonjwa ndani waleteni wakapate matibabu," alisema Mbwambo.

Alisema kuna wagonjwa wengi majumbani lakini hawajitokezi kupata matibabu ya ugonjwa huo.

Alibainisha hivi sasa matibabu yote yanapatikana katika hospitali hiyo, hivyo jamii isifiche wagonjwa majumbani badala yake wawapeleke wagonjwa kupata matibabu.

Mbwambo alisema wagonjwa wa kiharusi wapo wengi hivyo wanapaswa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya ili kupata matibabu sahihi.

Katika hatua nyingine, Mbwambo alisema wanaendelea kutoa matibabu kwa wagonjwa wa moyo kwa watu wazima na watoto kutokana na serikali kuwekeza huduma za kibingwa kwenye hospitali hiyo.

Alisema: "Tuna kliniki ya wagonjwa wa moyo pamoja na magonjwa wengine kwa ajili ya kupata matibabu ya magonjwa mbalimbali, tuna kitengo cha utoaji wa matibabu ya moyo nasisitiza wananchi wasikubali kurubuniwa kwenda kutibiwa kienyeji."

# Askofu awashauri CHADEMA kuhusu maandamano

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Kanisa la Maombi na Maombezi kwa Mataifa yote (RUTACH), Askofu Living Mwambapa, amekishauri Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutafuta njia sahihi ya kuwasilisha hoja zao na kutafutiwa ufumbuzi na siyo kufanya maandamano.

Mwambapa alitoa kauli hiyo juzi mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kauli ya CHADEMA kutaka kufanya maandamano ya amani nchi nzima kushinikiza serikali kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa uchaguzi.

Askofu huyo alisema Watanzania wanatakiwa kuhamasishwa kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo zinazoelekezwa na serikali kwa ajili ya taifa na siyo kupoteza muda kwa ajili ya maandamano kwa maslahi ya wanasiasa.

"Watanzania msidanganyike na wanasiasa wanaowahamasisha kuivuruga amani iliyopo wakati wao wenyewe na familia zao hawapo na wamejifungia majumbani mwao."

"Kwa jinsi ninavyowatazama hao CHADEMA lengo lao ni kuvuruga amani ya nchi kwa faida zao binafsi na wanafana chokochoko ili serikali ivurugike kwa kuamini kuwa watanufaika wakati wanajidanganya na kupoteza muda wao," alisema.

Hivyo, aliwahimiza Watanzania kutunza na kudumisha amani iliyopo kwa ustawi wa taifa lao.



# Nyanda za Juu Kusini kinara matumizi dawa za kulevya

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MIKOA ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imetajwa kukithiri kwa matumizi ya dawa za kulevya na biashara kutokana na kuwa na mwingiliano mkubwa na raia wa nchi jirani.

Hayo yalisemwa juzi na maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (DCEA) wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walipokuwa wanatoa elimu ya kupambana na dawa za kulevya kwa wanafunzi wa Chuo cha Uwalimu Mpuguso kilichopo wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya.

Ofisa Elimu wa DCEA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Adrick Ndelwa, alisema uingiaji na utokaji wa dawa hizo katika mikoa hiyo unakuwa rahisi kutokana na mikoa hiyo kuwa mpakani.

Alisema kutokana na hali hiyo wameamua kuanza kutoa elimu ya kupambana na dawa hizo kwa makundi mbalimbali ya jamii hasa vijana ili wajuwe madhara ya matumizi ya dawa hizo na waepuke kujiingiza kwenye makundi yanayotumia.

Alisema wameanza kutoa elimu hiyo kwa kuanzia kwenye vyuo vikuu na vyuo vya kati na kwamba baada ya hapo wataanza kwenda kwenye shule za sekondari na msingi ili kuhakikikisha vijana wote wanafikiwa na elimu hiyo.

"Lakini pia tutapita kwenye taasisi zote za dini na maeneo yote ambayo vijana wanapatikana ili kuhakikisha elimu hii inafika kwa usahihi na vijana wanaepuke kutumia dawa hizi kwa sababu madhara yake ni makubwa," alisema Ndelwa.

Mwanasheria wa DCEA Kanda, Denastus Mnyika, alisema vita ya dawa za kulevya ni vita ya kimataifa kwa maelezo kuwa Tanzania inashirikiana na mataifa mbalimbali duniani kupambana na matumizi ya dawa hizo.

Aliwataka Watanzania wote kushiriki kwenye vita ya dawa hizo kwa kuhakikisha wanatoa taarifa ya watu wanaozitumia ili kuwadhibiti mapema kabla hazijawaletea madhara yakiwamo ya kiafya. Alisema biashara ya dawa za kulevya na matumizi yake ni kinyume na sheria za nchi na hivyo akawataka vijana kuepuka kuzitumia ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria.

"Tunatoa elimu hii kwa vijana kwa sababu hili ndilo kundi kubwa ambalo linaathirika na matumizi ya dawa hizi, lakini mbali na elimu pia tunachukua hatua za kisheria dhidi ya wale wanaokutwa wakifanya biashara ya dawa hizi.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Mwalimu Edes Kaulule, alisema katika chuo hicho kuna viashiria vya baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho kutumia dawa za kulevya na hivyo akawashukuru maofisa wa DCEA kwa kuanza kutoa elimu.

Alisema baadhi ya vijana hao huwa wanaonyesha tabia ambazo zinafanana na za wanaotumia dawa za kulevya na hivyo akawasisitiza kuacha.

Kaulule alisema: "Hatujathibitisha kwamba wanatumia lakini kuna viashiria, kwa hiyo niwaombe sana vijana muepuke sana matumizi ya dawa hizo na kwa wale ambao mmeanza kutumia semeni ili msaidiwe namna ya kuacha."



Ofisa Elimu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Adrick Ndelwa, akitoa elimu ya madhara ya dawa za kulevya kwa wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mpuguso kilichoko Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima parachichi waanzisha 'saccos' kukopeshana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa maparachichi mkoani Njombe wameanzisha chama cha kuweka na kukopa kwa ajili ya kusaidia wakulima wadogo ambao hawana vigezo vya kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.

Hivyo kinawapatia mikopo kwa riba na masharti nafuu kwa lengo la kuendeleza kilimo hicho.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Asasi ya Wakulima wa Parachichi Nyanda za Juu Kusini (NSHIDA), Frank Msigwa, kwenye mkutano mkuu wa wakulima wa zao hilo uliofanyika mkoani Njombe.

Alisema sababu ya kuanzisha Saccos hiyo ni kuwa asilimia 95 ya wakulima wa parachichi mkoani humo hawana sifa ya kukopesheka kwenye benki.

Msigwa alisema wamefanya juhudi za kuunganisha wakulima na benki lakini ni asilimia tano pekee ndiyo yamefanikiwa kupata mikopo na haswa ni wakulima wakubwa ambao wana uwezo.

Alisema wakulima wanastahili kukopesheka kwasababu wana uwezo wa kulipa kwa kuwa masoko ya uhakika yapo.

Alisema Njombe kuna zaidi ya kampuni 15 yamefika kwa ajili ya kununua parachichi, hivyo mkulima akiwezeshwa kwenye miundombinu ya maji, pembejeo na dawa atazalisha parachichi iliyo bora na kuuzika kirahisi.

Hata hivyo waliomba Wizara ya Kilimo kuwaongezea nguvu ili wakulima waweze kupata mitaji ya kuendesha shughuli za kilimo.

Ofisa Ushirika wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Idd Chamshama, alisema serikali inatambua kuwa ushirika ni nyenzo muhimu ya kuwezesha wananchi kiuchumi hasa wakulima wadogo.

Chamshama alisema jukumu la serikali ni kuendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha vyama vya ushirika kwa malengo ya kujikomboa na umaskini na kuboresha maisha yao.

"Kwa hiyo serikali kupitia sera ya maendeleo ya ushirika inahimiza uanzishwaji wa vyama vya ushirika ambavyo ni imara na endelevu vitakavyokidhi matarajio ya wanachama," alisema Chamshama.

Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, Alatanga Nyagawa, alisema ili wakulima wa parachichi mkoani Njombe waweze kukua kiuchumi na kutatua changamoto zinazowakabili ni lazima waungane.

"Fursa tulizonazo kwenye parachichi ni lazima tuitumie kwa kutafuta masoko ya uhakika ili wakulima wetu wakue kiuchumi," alisema Nyagawa.

Baadhi ya wakulima wa parachichi mkoani Njombe akiwamo, Tumaini Mhoka alisema kuanzishwa kwa chama hicho kitawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuwa na masoko ya uhakika.

Alisema: "Ukienda benki unaambiwa ulete dhamana sasa wewe ni mkulima ndiyo unaanza na wanataka hati sasa wengi wetu hatuna na wakati mwingine ukifanikiwa kuchukua mkopo mwezi unaofuata unaambiwa uanze kulipa wakati unategemea ulime, uvune kisha ndiyo uuze na kulipa madeni".

# Matumizi mabaya mitandao yamkera M/kiti CHADEMA

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANACHAMA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya wametakiwa kuacha matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ikiwamo kutoa taarifa za uzushi dhidi ya viongozi wa chama hicho.

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote maarufu kwa jina la China wa China ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Kanda ya Nyasa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wanachama wa chama hicho wa Wilaya ya Kyela.

Alikemea vitendo hivyo ikiwa ni siku chache baada ya baadhi ya wanachama wa chama hicho kuandika taarifa za uzushi kwenye mitandao wakieleza kuwa amevuliwa nyadhifa zote ndani ya chama hicho na kufukuzwa uwanachama.

Alisema taarifa hizo zilikuwa ni za uzushi na zilienezwa na watu ambao wanataka kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho ikiwemo nafasi ya mwenyekiti wa mkoa na kwamba wameamua kuanza kumchafua.

"Hizi taarifa za uzushi siyo mara ya kwanza kutolewa, nawaomba wanachama wa CHADEMA wanaotaka nafasi za uongozi ndani ya chama wafuate kanuni na taratibu za chama," alisema Mwasote.

Alisema uongozi haupatikani kwa kuwachafua wengine bali kwa kukubalika na wanachama ambao ndiyo wapiga kura na ndio wanaochagua kiongozi wanayeona anawafaa.



# Waziri aagiza upatikanaji vifaa, mbinu bora ufundishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amewataka walimu na wasimamizi wa Taasisi ya Microtech of Business na Technology kutafuta vifaa na mbinu bora za kufundishia zitakazokwenda sambamba na sayansi na teknolojia.

Amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia wanafunzi kuwa bora na kushindana katika soko la ajira la Afrika Mashariki.

Alitoa wito huo juzi wakati wa mahafali ya tano ya taasisi hiyo yaliyofanyika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema kuwa sasa hivi kuna ushindani mkubwa wa ajira, hivyo ni vyema taaluma ambazo wanatoa zizingatie soka la ajira la Afrika Mashariki.

Makame alisema kuwa ni aibu kubwa kuona katika maeneo mengi kuna wageni na Wazanzibari wapo nyuma akisema hali hiyo ifike mwisho.

Sambamba na hayo aliwataka wazee na walezi kujitahidi kulipia ada kwa wakati, kwamba kutokulipa ada ni kudhoofisha upatikanaji wa taaluma kwa vijana wao.

Alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo yana lengo la kutengeneza fursa za ajira pamoja na kukuza uchumi wa ndani ya nchi yao.

Mkuu wa Chuo hicho, Farhiya Mohamed Aliy, alisema kuwa mafanikio yote ambayo yamepatikana ndani ya chuo chao, yasingweza kufikiwa kama kusingekuwa na mchango wa serikali.

Alisema kuwa chuo kinatoa fani mbalimbali ambapo katika mahafali hayo wahitimu 191 wamehitimu masomo yao kwa ngazi ya cheti na stashahada wakiwamo wanawake 137 na wanaume 54.

Naibu Mwenyekiti wa chuo hicho, Dk. Omar Said, alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho miaka tisa wameshatoa wahitimu 765 wakiwamo wanawake 549 na wanaume 224.

# Serikali yatakiwa kufanya tathmini uhamishaji, marekebisho pensheni jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Sabiha Filifil Thani, amesema serikali inapaswa kufanya tathmini kuhusu marekebisho waliyofanya ya kuhamishia pensheni jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwenda Wizara ya Fedha.

Amesema kwa sasa kuna changamoto nyingi baada ya kuhamishwa kwa pensheni hiyo.

Akizungumza na viongozi na watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alisema kuwa wamepokea malalamiko mengi kutoka kwa wazee kuhusu pensheni hiyo.

Thani alisema kipindi cha miezi sita inatosha kufanyiwa tathmini ili kuona pale ambapo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa wazee wao na ifanyike kwa hatua ya pili ambayo Wizara ya Fedha imeweza kutekeleza utaratibu huo.

Aliema kuwa hatua hiyo itabaini changamoto zilizojitokeza kwa sekta zote mbili na kupata kujua ni nani hasa ataweza kupewa fursa ya kuwahudumia wazee ili kuondokana na changamoto ambazo wazee walizielezea.

"Haiwezekani kwamba mzee anafursa ya kupata fedha lakini zinafika miezi sita hajapata hata mwezi mmoja na anapokwenda kufuatilia anaambiwa aende kushoto, mzee hana nguvu, hana mwelekeo kuanza kumzungusha huku na huku anaamua kukata tamaa wakati ile ni haki yake," alisema.

Wakizungumza na waandishi wa habari baadhi ya wazee ambao walikutana na kamati hiyo, Amoir Haji na Fatma Mussa, walisema kuwa tangu pensheni jamii kuhamishiwa Wizara ya Fedha kumekuwa na changamoto nyingi ikiwemo kukosa fedha zao, kuhamishiwa vituo bila ya taarifa na kubadilishiwa tarehe na kupata usumbufu.

Aidha wazee hao walisema kuwa suala la fedha zao kuhamishiwa benki pia ni usumbufu kwao kutokana na makato mengi.

Aidha aliitaka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufanya utafiti wa kina kujua ni vikundi vingapi vya wajasiriamali vinafaa kuhusika na fursa ya kupatiwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuviendeleza.

Alisema katika taarifa ya wizara hiyo kuna Sh. bilioni 33.8 ambazo zipo katika mpango wa miaka minne ambazo ni za mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB).

Alisema kuwa katika maelezo hayo fedha hizo zitakwenda katika uwezeshaji kiuchumi kwa wajasiriamali wanawake, kupambana dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Aidha alisema kutokana na changamoto ya penSheni jamii ipo haja serikali kufanya tathmini kuona pale wizara hiyo ilipokuwa inatekeleza pensheni hiyo kwa wazee.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha miezi sita kutoka Julai hadi Disemba 2023, Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema wizara yao imebuni mbinu muafaka itakayoweka utaratibu bora utakaohakikisha taarifa za wazee watarajiwa zinapatikana, kuingizwa katika mfumo endelevu wa elektroniki.

Alisema kuwa hilo linafanyika baada ya kuwapo kwa changamoto ya kuwepo kwa ongezeko la malalamiko kwa wazee ambao wananufaika na mpango wa pensheni jamii.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Premier Enterprise, Humud Nassor, akionesha mafuta wakati akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu taarifa za uzushi zilizosambazwa katika baadhi ya mitandao ya kijamii kuwa mafuta hayo yamekatazwa duniani kote. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni yalia kuhujumiwa katika mitandao ya kijamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMPUNI ya Premier Enterprise inayojishughulisha na kuuza na kusafirishaji bidhaa ikiwamo mafuta ya kupikia, imekanusha taarifa zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii ya kwamba bidhaa yao ya mafuta ya dyanas imepigwa marufuku.

Akizungumza na waandishi wa habari jana visiwani hapa, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Humud Nassor Humud alisema taarifa hizo ni potofu na zimelenga kuathiri biashara yao.

Alisema mafuta hayo huteremshwa baharini kwa nia ya kupakiwa kwenye vyombo vya usafiri na siyo kwa ajili ya kutoa nembo kupitia njia ya maji kama ilivyoelezwa katika taarifa za uzushi zilizosambazwa mitandaoni.

"Mafuta ya dyanas hajapigwa marufuku sehemu yoyote duniani hivi ni vita tu vya kibiashara lengo lao kutuharibia biashara zetu lakini taarifa hizi tushazipelekea katika taasisi husika ili kufanyiwa uchunguzi na kubainika kwa aliyesambaza taarifa hizi na kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Alisema kampuni hiyo imeshawasiliana na wakili wake na itafuatilia kwenye vyombo vya serikali kama Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ili kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa kwa aliyehusika.

Alisema hakuna changamoto ya upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya kula na bidhaa hiyo ipo kwa wingi.

Alisema kampuni hiyo imesajiliwa mwaka 2011, inaagiza mafuta kutoka nchini Malaysia, inauza na kusafirisha Zanzibar na Tanzania Bara. Alisema mafuta hayo yanaingia nchini kihalali na kuthibitishwa na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS) pamoja na taasisi zote za kiserikali zinazoshughulikia uingizaji halali wa mafuta ya kupikia nchini.

# Othman ahadharisha Watanzania viongozi wapenda madaraka, ubinafsi

**Na Mwandishi Wetu, IKWIRIRI**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewatahadharisha Watanzania kuchagua viongozi wenye nia ya kutafuta jimbo na baadaye kwenda kutumia vibaya madaraka. Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, ameyasema hayo kwa nyakati tofauti Ikwiriri, mkoani Pwani katika mkutano wa hadhara na ufunguzi wa mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa chama hicho ngazi ya mikoa unaoendelea nchini kote.

Alisema viongozi wanaohitajika ni wenye uwezo wa kujitoa na kujitolea na pia kuwashajiisha wenzao kuhakikisha nchi inapata mafanikio kwa kuzisikiliza kero za watu na kuzipatia ufumbuzi badala ya kufikiria utajiri binafsi.

Alisema viongozi wanaoendekeza ubinafsi wataifanya nchi kutoweza kuzitumia rasilimali kwa manufaa ya Watanzania na badala yake kuendelea na aibu ya kupiga magoti kuomba msaada katika nchi ambazo zinaonekana tajiri, lakini zenye rasilimali chache kuliko ulivyo mkoa mmoja wa Tanzania.

Alisema ukiachwa wa Mkoa wa Ruvuma, Pwani ina uwezo mkubwa wa maji ambayo pekee kama yataweza kutumiwa vyema yana uwezo wa kuzalisha kilimo cha bidhaa za kuzalisha mafuta ya kula na sukari ya kutosheleza mahitaji ya Tanzania kwenye eneo hilo bila kuagiza kutoka nje.

Othman alisema viongozi wabovu wanashindwa kuzishughulikia kero mbalimbali za wananchi jambo ambalo linahitaji kufanyiwa mabadiliko kwa kuchagua viongozi wenye uwezo na uchungu wa nchi yao katika kuleta maendeleo.

Kadhalika, wananchi ndio wenye uwezo wa kufanya mageuzi na ni jambo linalowezekana iwapo wataungana pamoja kuhakikisha nchi yao inasonga mbele kiuchumi na kimaendeleo.

Aidha, viongozi wenye juhudi ya kutafuta mafanikio ya taifa lao ndio wanaohitajika kuungana na wananchi ili taifa lao liweze kusonga mbele na kuondokana na umaskini kwa kuwa taifa la Tanzania lina kila aina ya rasilimali na utajiri mkubwa wa kila aina.

Aliwataka viongozi wanaochaguliwa kuwa na mwenendo wa tabia za uongozi na kutotoa siri za vikao vinavyofanyika kwa kuwa kufanya hivyo kunarejesha nyuma maendeleo ya chama na taifa kwa jumla.

Akiwa ziarani Ikwiriri alifungua matawi matatu ya chama hicho ikiwa ni jitihada za viongozi wa chama hicho kuendeleza ujenzi wa chama kukifanya kuwa taasisi imara na pia kuweka alama ya chama hicho nchini kote.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Kuluthumu Jumanne Mchuchuri, alisema wananchi wa Mkoa wa Pwani wamekabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo za afya, kiuchumi, elimu na kijamii ambazo zinahitaji viongozi makini na wenye uzalendo katika kupambania shida za wananchi.

Aliwaonya wananchi wa jimbo hilo kutochagua viongozi wanaoendeleza ubinafsi na fitna za wenyewe kwa wenyewe jambo linaloweza kuhatarisha taifa.



Ukarabati wa daraja la Kunduchi wilayani Kinondoni ukiendelea baada ya kuzolewa na maji ya mvua inayoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

# Vifo vya uzazi Arusha vyapungua kwa miaka miwili

**Na Christina Mwakangale, ARUSHA**

VIFO vitokanavyo na uzazi, vimepungua mkoani Arusha, kutoka 61 mwaka 2021 hadi kufika 39 mwaka 2023.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa, aliyasema hayo jijini hapa, mbele ya maofisa kutoka Wizara ya Afya, TAMISEMI pamoja na waandishi waliokatika ziara ya kubaini mafanikio katika sekta hiyo ya Mfuko wa Afya wa pamoja nchini (Health Basket Fund-HBF), baada ya maboresho ya miundombinu, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Dk. Mkombachepa, alisema kuanzia mwaka 2022/2023, mkoa umefanikiwa kuwaokoa kinamama wenye matatizo ya dharura za uzazi 2,555 ambao walipatiwa huduma na kuondoa hatari ya vifo.

"Wajawazito 12,719 (18.5%) kati ya 68,688 walijifungua kwa njia ya upasuaji katika vituo 21 vinavyotoa huduma za upasuaji. Vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka 61 mwaka 2021 hadi 39 mwaka 2023.

"Mkoa wa Arusha una jumla ya wilaya sita na halmashauri saba. Jumla ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya serikali ni 259 kwa halmashauri zote. Zahanati zimeongezeka kutoka 194 mwaka 2021/22 na kufikia 211 mwaka 2022/23," alisema Mganga Mkuu.

Kadhalika, huduma za upasuaji katika vituo vya afya imeongezeka kutoka 17 hadi 22. Hospitali za halmashauri za wilaya zinazofanya kazi zimeongezeka kutoka tatu mwaka 2021/22 hadi saba mwaka 2022/23.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema huduma za afya mkoani hapa, ikiwamo bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 14 iliyotumika katika ununuzi wa vifaa tiba, ujenzi miundombinu, umesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Alisema fedha za HBF pamoja na za wadau wengine ikiwamo mradi wa huduma ya M-MAMA imeokoa wajawazito 2,555 ambao walipatiwa huduma ya dharura na wengine wakifanyiwa upasuaji katika vituo vilivyoanza kufanya upasuaji.

"Fedha hizi za HBF pamoja na miradi mingine imefanya ongezeko la upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 66 hadi 93 kwa kipindi cha miaka miwili, 2022/2023," alisema Mongella.

# Wanaoajiri raia kigeni kinyemela waonywa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKULIMA wa tumbaku mkoani Shinyanga, wameonywa tabia ya kuajiri raia wa kigeni kinyemela kutoka nchi ya Burundi na kuwatumikisha kwenye kilimo hicho bila vibali vinavyotolewa na Idara ya Uhamiaji.

Ofisa wa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, Salumu Rashidi alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza na wakulima zaidi ya 200 waliohudhuria Mkutano Mkuu wa 28 wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU).

Alisema, kuajiri raia wa kigeni bila kibali ni kosa kisheria, mwajiri akibainika anafunguliwa kesi ya jinai na kufikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria za Uhamiaji na kuwataka kuacha mara moja tabia ya kuwaingiza wageni hao kwa njia za panya.

Aidha, alisema Sheria ya Uhamiaji sura 54 marejeo ya 16 kifungu cha 45 kifungu kidogo cha kwanza kinaeleza kuwa ni kosa kumwajiri raia wa kigeni na adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 500,000 au kifungu kisichozidi miaka mitatu jela na kuwasihi kuzingatia sheria za kuwapata vibarua shambani.

Rashidi alisema, watakaokidhi vigezo watapata vibali hivyo na lazima awe raia wa nchi jirani, hati ya kusafiria, uthibitisho kutoka serikali ya mtaa na kijiji, kujaza fomu maalum na mwajiri ndio anawajibika kufuatilia kibali hicho cha miezi mitatu kinachogharimu Sh. 30,000 na miezi sita Sh. 60,000 na kinatolewa kwa msimu pekee.

"Halmashauri yetu ya Ushetu tunafahamu inategemea mapato yake kupitia kilimo cha Tumbaku na pamba kwa kiwango kikubwa, hatutakiwi kuwa sehemu ya kudhoofisha upatikanaji wa mapato kwa kuwakata wakulima hivyo ni vyema mkazingatia sheria ya kupata vijakazi shambani," alisema Rashidi.

Ofisa wa TAKUKURU, Frank Masilamba, aliwataka Mwenyekiti na wahabasibu wa vyama vya msingi (AMCOS) kuandaa taarifa za kuomba mikopo benki ambazo zina uhalisia wa uhitaji wa wakulima wao badala ya kuongeza mahitaji ambayo hayahitajiki.

Aliwataka kukopa fedha kwa ajili ya mahitaji halisia ya wakulima wao ambazo nao watazilipa na kunufaika na uwapo wa kilimo wanachokifanya.

Aidha, alisema mwisho wa soko la tumbaku na pamba watapata uhakikisha anacholipa mkulima ndio kile kilichohitajika na wakikuta ni tofauti wahusika watawajibika.

Awali, akitoa taarifa ya ununuzi wa pamba, Meneja wa KACU, Abduly Ally alisema, zaidi ya kilo milioni 5.1 za mbegu za pamba zenye thamani ya Sh. bilioni 5.4 zilinunuliwa kutoka Kishapu, Kahama Manispaa, Msalala na Ushetu kwa fedha za mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo(TADB) kwa msimu wa 2023/2024.

HABARIKIMATAIFA

# Ousmane Sonko azuiliwa kugombea urais Senegal

**DAKAR, Senegal**

BARAZA la Katiba nchini Senegal limemzuia kugombea urais kiongozi mkuu wa upinzani, Ousmane Sonko na mwanawe aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Abdoulaye Wade, baada ya majina hayo kutoonekana kwenye orodha ya majina ya wagombea 20 watakaoshiriki katika uchaguzi wa Februari mwaka huu.

Kwa mujibu wa orodha hiyo iliyotolewa jana waaliotajwa kushiriki katika kinyang'anyiro hicho cha urais ni Waziri Mkuu wa sasa, Amadou Ba ambaye aliteuliwa na Rais Macky Sall kama mrithi wake pale alipotangaza mwezi Julai kwamba hatosimama kwenye uchaguzi huo kuwania muhula wa tatu.

Inaelezwa kuwa katika orodha hiyo wametajwa pia mawaziri wakuu wawili wa zamani ambao ni mahasimu Idrissa Seck na Mahammed Dionne, meya wa zamani Khalifa Sall na Bassirou Faye ambaye ni mbadala wa Sonko.

Kiongozi wa upinzani Ousmane Sonko aliyechukuwa nafasi ya tatu katika uchaguzi wa rais wa mwaka 2019 amekuwa katikati ya mvutano mkubwa na dola, mvutano uliodumu kwa zaidi ya miaka miwili sasa na umezusha machafuko mara kwa mara yaliyosababisha umwagaji damu nchini Senegal.

Mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 49 alijipatia umaarufu mkubwa nchini Senegal na hasa miongoni mwa vijana akijulikana zaidi kwa misimamo yake ya kutetea ushirikiano na mshikamano wa Waafrika na kusimama imara dhidi ya Ufaransa iliyokuwa mkoloni wa zamani wa taifa hilo.

SABABU KUONDOLEWA

Ilibainishwa kuwa Baraza la Katiba limemwondowa Sonko kwenye orodha ya wagombea kutokana na kifungo cha nje cha miezi sita alichohukumiwa kutokana na kesi ya tuhuma za kumchafulia jina Waziri wa Utalii, Mame Niang, ambayo pia iliungwa mkono na mahakama ya juu Januari nne, mwaka huu, pamoja na kutozwa faini kubwa.

Inaelezwa kuwa kiongozi huyo wa upinzani mwezi Juni 2023, katika kesi nyingine alihukumiwa kifungo cha miaka miwili kwa kudaiwa kuwapotosha vijana kimaadili na tangu mwishoni mwa mwezi Julai yuko jela kutokana na mashtaka mengine ikiwamo kuitisha uasi, kushirikiana na makundi ya kigaidi na kuhatarisha usalama wa taifa.

Aidha, ilielezwa kuwa Sanko alikanusha mashtaka yote hayo akisema yametengenezwa kwa lengo la kumzuia kugombea uchaguzi wa rais mwezi Februari, tuhuma ambazo serikali inazipinga.

Orodha ya wagombea urais iliyochapishwa Jumamosi inajumuisha pia majina ya wanawake wawili, daktari wa magonjwa ya wanawake Rose Wardini na mfanyabiashara Anta Babacar Ngom.

Kwa mujibu wa mwanasheria wa masuala ya katiba Babacar Gueye, hiyo ni mara ya kwanza kwa Senegal kuandaa uchaguzi wa rais utakaokuwa na orodha ndefu ya wagombea. Ikielezwa kuwa katika uchaguzi wa 2019 kulikuwa na wagombea watano tu wa kiti hicho.

**DW**



Wasichana wa familia moja waliookolewa jana na polisi baada ya kutekwa nyara huko Nigeria, wa pili kushoto ni Nabeeha anayedaiwa kuuawa na watekaji hao. **PICHA: MTANDAO**

# Polisi yaokoa familia iliyotekwa Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

JESHI la Polisi nchini Nigeria limesema limefanikiwa kuwaokoa dada watano waliokuwa wakishikiliwa mateka baada ya kutekwa nyara Mjini Abuja na kwamba waliachiliwa wakati wa operesheni ya jeshi hilo katika msitu wa kaskazini mwa nchi hiyo.

Polisi walieleza jana kuwa mabinti hao walichukuliwa kutoka nyumbani kwao huko Abuja mapema mwezi huu, pamoja na dada mwingine ambaye aliuawa baadaye. Na kwamba watekaji nyara walikuwa wamedai fidia ili waachiliwe, lakini taarifa hiyo haikutaja iwapo kuna mtu aliyelipwa.

Pia polisi hao walisema wasichana hao walikuwa wamerejea tena kujiunga na familia yao kufuatia operesheni hiyo, iliyofanyika karibu na msitu wa Kajuru katika Jimbo la Kaduna juzi.

Ilielezwa kuwa wasichana hao wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 18 hadi 23 walichukuliwa mateka pamoja na baba yao, Mansoor Al-Kadriyar, Januari 2, mwaka huu katika nyumba ya familia huko Bwari, Kitongoji cha Abuja.

Walioshuhudia walisema mjomba wa wasichana hao alikimbia kutafuta usaidizi lakini aliviziwa na kuuawa, sawa na maofisa watatu wa polisi.

Watekaji nyara walimwachilia Mansoor kwa sharti la kupata fidia kubwa, lakini binti yake mwenye umri wa miaka 21, Nabeeha, mwanafunzi wa mwaka wa mwisho wa chuo kikuu, aliuawa kama onyo, kulingana na mwanafamilia aliyezungumza na BBC kwa sharti la kutokujulikana.

**BBC**

## Russia yaonyesha wasiwasi dhidi ya Magharibi

**MOSCOW**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara wa Russia, Denis Manturov, ameonyesha wasiwasi juu ya juhudi za Magharibi kukusanya taarifa zinazohusu uzalishaji na ulinzi wa taifa hilo kwa kulenga wataalamu wa kisekta, akieleza kuwa hiyo inamaanisha kuwa huo ni mpango unaoratibiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na waziri huyo jana, kuwasiliana na wataalamu kwa habari inaweza kuwa mbinu ya kimkakati zaidi kwa wapelelezi kuliko kushirikiana na askari, ambao ni mahiri zaidi katika kugundua ujasusi.

Alisema mashirika ya kijasusi ya nchi za Magharibi yanafahamu vyema mbinu hiyo, kwakuwa yamekuwa yakiitumia wao kwa wao, akieleza kuwa ujasusi wote unalenga kupata manufaa ya kiuchumi, iwe katika migogoro au vita, na kwamba matokeo yake huathiri nafasi za kiuchumi za siku zijazo.

"Suala la mzozo wa kijeshi kati ya Russia na muungano wa kijeshi wa Magharibi kupitia Ukraine linafunika ukweli kwamba, wakipewa fursa, viongozi wa nchi za Magharibi wangetanguliza maslahi ya kiuchumi badala ya ushirikiano. Mzozo wa Ukraine umesisitiza mtazamo wa Ujerumani kama mpinzani wa kiuchumi mbele ya Marekani," alisema.

Aliongeza kuwa ushindani huo ulioonekana katika ukosoaji wa Washington wa bomba la gesi la Nord Stream la Ujerumani kabla ya usumbufu wake wa kushangaza. Akielezwa kuwa hali ya sasa inahusisha Marekani inayoshawishi makampuni ya Ujerumani kuhama kwa motisha ya kodi ya kijani na nishati ya kutosha na kuchangia katika uondoaji wa viwanda vya Ujerumani.

Aidha, alieleza kuwa mwaka wa 1995, gazeti la Los Angeles Times liliripoti kwamba utawala wa Rais Bill Clinton uliiagiza CIA kuondoa ujasusi wa kiuchumi na kwamba hata kabla ya Clinton, ilionekana wazi kuwa ushindani wa kiuchumi na mataifa makubwa ya kiviwanda kama Japan na Ujerumani ulikuwa ukifanyika.

# SERIKALI, USAID WAITA MASHABIKI MECHI AFCON, KUPIMA AFYA BURE

**Na Mwandishi Wetu**

KWA juhudi za pamoja, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na mradi wa USAID Breakthrough ACTION, imezindua maonyesho ya kukutanisha wananchi kuangalia mechi za Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), huku ikiwapatia huduma mbalimbali za afya kama chanjo, upimaji wa VVU na elimu ya afya kwa ujumla.

Kampeni hii ya kipekee, inayoratibiwa na shirika la Johns Hopkins Centre for Communication Program, kupitia mradi wa Breakthrough ACTION, unaofadhiliwa na USAID, ina lengo la kuchochea fursa kwa Watanzania kuboresha afya zao kupitia kubadilisha mila na desturi hasi ili kuboresha afya.

Onyesho la kwanza lilifanyika mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Zakheim Mbagala, mgeni rasmi akiwa Dk. Festo Dugange, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Dk. Dugange alihamasisha mashabiki wa mpira wa miguu, hasa wanaume kuangalia familia zao kama timu.

"Na ili kujipatia ushindi, inabidi tuwe mstari wa mbele katika kuhakikisha familia zetu zinajikinga na magonjwa mbalimbali kwa kupata chanjo kulingana na mahitaji," Dk. Dugange alisisitiza na kuongeza kuwa chanjo ni salama na zinatoa kinga madhubuti dhidi ya magonjwa.

Dugange aliendа mbele zaidi na kuhamasisha wananchi kutumia huduma zinazotolewa viwanjani hapo kama vile, chanjo za watoto, chanjo za mabinti za kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi, pamoja na chanjo za UVIKO-19 sambamba na kuwataka wananchi kupima Virusi vya UKIMWI (VVU), na kutumia kondomu ili kujikinga dhidi ya maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

Kampeni hiyo pamoja na kufurahia mashindano ya AFCON, lakini pia inatumika kama jukwaa enezi la kuhamasisha afya na ustawi wa jamii, likisisitiza umuhimu wa kupata chanjo kulingana na mahitaji.

"Leo tumekutana kwenye onyesho hili muhimu linalolenga kupata elimu na huduma muhimu za chanjo, huku tukiburudika na kusubiri kwa hamu kuangalia mechi za AFCON. Natoa wito kwa wote mnaonisikiliza, hasa wanaume wenzangu, naomba muangalie familia zenu kama timu," alisema.

Aliongeza kuwa ni muhimu watu wote kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha familia zinajikinga na magonjwa mbalimbali kwa kupata chanjo kulingana na mahitaji yao na kwamba nchi ina chanjo zote muhimu na zinatolewa bure kabisa.



Msanii chipukizi wa nyimbo za singeli, Chiro, akitoa burundani kwa mashabiki wa mpira wa miguu kwenye Uwanja wa Mbagala Zakhem, Dar es Salaam wiki iliyopita. Maonyesho hayo yanakutanisha wananchi kuangalia mechi za Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), huku wakipata huduma mbalimbali za afya kama chanjo, upimaji wa VVU na elimu ya afya kwa ujumla. **PICHA: HISANI YA BREAKTHROUGH ACTION**

# Lala salama Ligi Kuu Z'bar kuanza Februari

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar mzunguko wa lala salama unatarajiwa kuanza Februari 2, mwaka huu.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), ilisimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo ilimalizika mapema Januari 13, mwaka huu kwa Mlandege FC kubeba ubingwa huo.

Hadi ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, inaishia mzunguko wa kwanza ulikuwa umetamatika kwa timu ya JKU kukaa kileleni na alama zake 36, ikifuatiwa na Zimamoto iliyohitimisha na pointi 30.

Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Issa Kassim, akizungumza na mwandishi wetu huko ofisini kwake Mbuyu Mnene mjini hapa, alisema tayari maandalizi kwa ajili ya kuendelea na ligi hiyo yamekamilika. Alisema katika mzunguko huu matarajio yao ni kuhakikisha makosa au changamoto ambazo zilijitokeza katika mzunguuko wa kwanza hazijirudii tena.

"Tumejipanga kwa kila hali ili kuona mzunguko huu unamalizika salama pasipo na malalamiko, mzunguko wa kwanza malalamiko mengi yalikuwa ni kwa waamuzi wa michezo, hivyo tumeyafanyia kazi na yataendelea kufanyiwa kazi wakati ligi ikiendelea", alisema.

Aidha, alisema kwa kuwa mzunguko huu ndio unaamua bingwa, wana uhakika utakuwa mgumu, lakini wanajipanga kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri hasa katika kusimamia kanuni.

Alieleza kuwa ili kuona ligi yao inamalizika vizuri kuliko misimu mingine, tayari wamekaa na kupanga mikakati ya kuhakikisha bingwa atapatikana kwa misingi ya haki.

Alisema imekuwa ni kawaida kila inapokuwa ligi inamalizika kutokea malalamiko ambayo mara nyingi huondoa ladha nzima ya ligi hiyo.

Hata hivyo, alisema katika msimu huu kama ambavyo hapo awali Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Suleiman Mahmoud Jabir, alivyotamka kuwa atahakikisha hakuna upangaji wa matokeo katika kumpata bingwa na ikibainika timu zitachukuliwa hatua, hilo ndilo watakalolisimamia ipasavyo.

## Yanga Princess, JKT Queens vitani leo

**Na Oliver Albert**

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara itaendelea leo kwa michezo mitano kupigwa kwenye viwanja tofauti hapa nchini huku mchezo unaosubiriwa na mashabiki wengi ukiwa kati ya Yanga Princess dhidi ya JKT Queens.

JKT ambao ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo, watakuwa wageni wa Yanga Princess kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi, wakati huo Alliance Girls ikiikaribisha Baobab Queens katika dimba la Nyamagana jijini Mwanza huku Bunda Queens wakiwa wenyeji wa Simba Queens kwenye Uwanja wa Karume Musoma.

Mchezo mwingine utaikutanisha , Geita Gold Queens dhidi ya Fountain Gate Princess katika Uwanja wa Nyankumbu Geita wakati Ceasiaa itakuwa mwenyeji wa Amani Queens kwenye dimba la Samora mjini Iringa.

Kocha wa Yanga, Mzambia Haalubono Charles, akizungumzia mchezo huo, alisema wamesahau matokeo ya mechi iliyopita na wanaingia kivingine kuhakikisha wanapata ushindi.

## Kikapu 13 waitwa Taifa michuano Afrika Mashariki

**Na Oliver Albert**

JUMLA ya wachezaji 13 wamechaguliwa kuunda Timu ya Taifa ya Mpira wa Kikapu kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kuanza Februari Mosi hadi 10 nchini Rwanda.

Msemaji wa Shirikisho la Mpira wa Kipau Tanzania (TBF), Marry Arthur, asema wamepokea mwaliko kutoka serikalini kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), likiwataka kuanza maandalizi kwa ajili ya ushiriki wa mashindano hayo.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi nane ikiwamo Tanzania, Uganda, Kenya, Sudan Kusini , DR Congo, Somalia, Burundi na wenyeji Rwanda.

„"Awali tulikuwa tuwe na mashindano ya Kombe la Taifa (Taifa Cup), Februari, lakini baada ya kuja kwa mwaliko huu wa kushiriki mashindano haya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, tukaona tusogeze mbele Taifa Cup hadi Juni 19, mwaka huu. „Hivyo tunaiomba mikoa yote itakayoshiriki Taifa Cup kuendelea kujiandaa kikamilifu ili ikifika wakati wa mashindano hayo ilete ushindani mkubwa kwa ajili ya kuzidi kukuza mchezo huu hapa nchini, „alisema Marry.

a

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BAYERN KUMKOSA TRIPPIER
KLABU ya Newcastle United imekataa ofa ya Bayern Munich ya kumnunua beki Kieran Trippier, 33. **(Sky Sports)**

### NEWCASTLE YAMGOMEA WILSON
KLABU ya Newcastle pia imekataa ofa ya mkopo kwa mshambuliaji wa England, Callum Wilson kutoka Atletico Madrid, lakini wanaweza kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ikiwa watapata ofa nono. **(Mail)**

### MOURINHO ATAKIWA SAUDIA
KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho, yuko kwenye mazungumzo na Klabu ya Saudia ya Al-Shabab kuhusu kuchukua nafasi ya ukocha baada ya kutimuliwa na AS Roma. **(Sportitalia)**

### CASEMIRO SASA KUUZWA
MUSTAKABALI wa kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro katika Klabu ya Manchester United baada ya msimu huu uko mashakani kwani klabu hiyo inaamini ni bora kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. **(Star)**

### BROBBEY KUTUA UNITED
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, ana nia ya kumleta mshambuliaji wa Ajax na Uholanzi, Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 21 pale Old Trafford wakati wa dirisha hili la Januari. **(Sky Sports)**

### LAPORTE AFUNGUKA SAUDIA
MLINZI wa Hispania, Aymeric Laporte, aliondoka Manchester City na kujiunga na Al-Nassr msimu uliopita wa majira ya joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amesema kuna wachezaji wengi ambao hawajaridhika kucheza kwenye Ligi ya Saudia. **(AS)**

### DE LIGT KUONDOKA BAYERN
MLINZI Matthijs de Ligt yuko tayari kuondoka Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto huku Manchester United wakifufua tena nia yao ya kumnunua beki huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24. **(Mirror)**

### SESKO KIPENGELE LEIPZIG
MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 20, ana kipengele cha kumruhusu kuondoka kwa pauni milioni 43 katika mkataba wake ambacho kitaanza kutumika msimu huu wa majira ya joto. **(Sky Sports)**

### DOUCOURE KUBAKIZWA EVERTON
KLABU ya Everton itaazimia kumshikilia kiungo wa kati wa Mali, Abdoulaye Doucoure mwenye umri wa miaka 31, ambaye anahusishwa na Klabu ya Al-Ettifaq huku klabu hiyo ya Saudi Pro League ikitafuta kuiziba nafasi ya kiungo wa kati wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, baada ya kuhamia kwake Ajax. **(Liverpool Echo)**

### ARSENAL HAITASAJILI JANUARI
KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, ametuliza matumaini ya mashabiki ya uwezekano wa shughuli nyingi za usajili katika dirisha hili la Januari, huku 'Washikabunduki' hao wakisita kulipa bei inayotakiwa kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, 27. **(Mirror)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AWATOA HOFU MASHABIKI KWA RICE

**Alihisi kubanwa na misuli, alipata usumbufu kutokana na kuchezewa rafu kipindi...**

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekiri Declan Rice alihisi „kubanwa" kwa misuli kabla ya kujiondoa mchezoni katika ushindi wao wa mabao 5-0 dhidi ya Crystal Palace kwenye Ligi Kuu England, Jumamosi.

'Washikabunduki' hao walikuwa mbele kwa mabao matatu na walisonga mbele wakati Rice alipoondoka uwanjani na nafasi yake kuchukuliwa na Jorginho.

Huku mashabiki wa Arsenal wakiwa hawajui kinachoendelea, Arteta alithibitisha baada ya mchezo huo kuwa kumtoa Rice ilikuwa ni tahadhari.

„Alikuwa akihisi kubanwa," alisema bosi huyo. „Sijui ilikuwa misuli gani. Lakini anaposema hivyo kwenye 3-0 basi ni wazi hatutaki kuchukua hatari yoyote."

Arsenal pia ilimpoteza beki wa kati Gabriel Magalhaes mwishoni mwa muda. Mlinzi huyo aliondoka uwanjani dakika ya 81 baada ya kukabiliwa na changamoto kali katika kipindi cha kwanza.

„Alipata usumbufu kutokana na kuchezewa rafu katika kipindi cha kwanza na alikuwa akijitahidi kidogo kwa hiyo ulikuwa wakati mwafaka wa kumtoa nje ya uwanja," alibainisha Arteta.

Gabriel alifunga kwa kichwa bao la ufunguzi la Arsenal siku hiyo akiunganisha kona na pia alifikiri kwamba alikuwa ameongeza la pili, lakini kipa wa Palace, Dean Henderson ndiye alijiyejifunga.

Leandro Trossard na Gabriel Martinelli kila mmoja alifunga baada ya mapumziko na Arteta alikiri kuwa alifurahi kuona wakipata ushindi mnono.

„Ukweli ni kwamba tulifanya mazoezi machache katika wiki iliyopita kuliko vipengele vingine vya mchezo," alisema Arteta.

„Huu ndio uzuri wake. Lakini tulifanyia kazi mambo mengi ambayo yalitokea na tuliwafundisha sana.

„Nimefurahishwa sana kumaliza mchezo huu bila kuruhusu bao, jambo ambalo tumekuwa tukikosa."

## HABARI MICHEZO



# KOCHA ASEMA TUNISIA HAIKUWA NA BAHATI

**KORHOGO, Ivory Coast**

KOCHA Mkuu wa Tunisia, Jalel Kadri, anahisi kwamba kikosi chake kilicheza vema, lakini hakikuwa na bahati ya kupata pointi zote tatu baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na Mali Jumamosi jioni kwenye Uwanja wa Amadou Gon Coulibaly huko Korhogo, Ivory Coast.

Mabingwa hao wa Afcon 2004 walitoka nyuma na kupata pointi moja kwenye mchezo wao wa pili wa makundi wa michuano ya Mataifa ya Afrika inayoendelea nchini Ivory Coast.

Akizungumza baada ya mechi hiyo mjini Korhogo, Kadri alisema pande zote mbili ziliendana vema, lakini akahisi walikuwa na nyakati bora zaidi ambazo zingewawezesha kushinda.

"Mechi ilikuwa ya nguvu sana, na tulihusika sana katika nyanja zote za mchezo. Tulikuwa tunatafuta ushindi, lakini hatukubahatika kuupata baada ya kucheza vizuri sehemu nyingi za mchezo.

"Timu zilikuwa sawa na dakika 10 za mwisho zilikuwa ngumu sana. Hatukuwa tunatafuta sare, tulijaribu kupata ushindi, lakini kwa bahati mbaya haikutokea," alisema Kadri.

Kadri aliongeza kuwa mchezo huo pia ulikuwa wa kimwili lakini ulitoa mtihani mzuri kabla ya mechi yao ya mwisho ya kundi hilo.

"Tulichoona leo (juzi) ni kwamba tulitoa mchezo mzuri. Walikuwa kimwili sana, na wachezaji wetu waligongwa lakini hilo halikutuzuia, na tuliendelea kucheza kwa bidii. Kupata pointi dhidi ya Mali ni muhimu sana na mechi ngumu kama hii ni nzuri kwetu kabla ya mechi ya mwisho ya kundi," aliongeza.

Tunisia wanajikuta katika hali ya tahadhari sana kuelekea mechi yao ya mwisho dhidi ya Afrika Kusini.

Kwa sasa wanakamata nafasi ya tatu kutoka kundi lao huku Mali wakiwa kileleni wakifuatiwa na Namibia ambao jana Jumapili walikuwa wakicheza na Afrika Kusini.

# Angola itafuzu16 – Bora: Pedro



**ABIDJAN, Ivoty Coast**

KOCHA Mkuu wa Angola, Pedro Goncalves, anatumaini timu yake itafuzu hatua ya 16 - bora baada ya ushindi wao mabao 3-2 dhidi ya Mauritania katika Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), juzi.

Palancas Negras (Swala) hao waliandikisha ushindi wao wa kwanza katika michuano ya Afcon dhidi ya Mauritania kwenye mchezo uliozalisha mabao matano.

Pamoja na ushindi huo, Goncalves aliimwagia sifa timu ya Mauritania kwa kucheza vizuri na kutoa upinzani mkali.

"Tulicheza dhidi ya timu kubwa ya Mauritania, bado watakuwa na mengi ya kuthibitisha, wao ni wapiganaji.

"Ilikuwa mechi ya kuvutia na ya kujitolea sana. Ushindi huu muhimu unatuwezesha kusonga mbele kwa tofauti nzuri ya mabao ikilinganishwa na Burkina Faso.

Ikiwa na pointi 4 na kileleni mwa Kundi D, Angola sasa inasaka kufuzu kwa awamu ya mtoano.

"Sasa tutajaribu kudumisha kasi kwa kutafuta kufuzu katika raundi inayofuata. Ningependa kutoa pongezi kwa wachezaji wangu waliojitolea vilivyo, huku nikiwa na subira.

"Tuna mpango wa kimbinu ulioainishwa vema ambao tutautekeleza kwa mechi dhidi ya Burkina Faso," aliongeza.

Angola itacheza na Burkina Faso katika mchezo wao wa mwisho wa Kundi D kwenye Uwanja wa Charles Konan Banny mjini Yamoussoukro kesho, Jumanne.

# Algeria waridhika kwa sare

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOCHA Mkuu wa Algeria, Djamel Belmadi, amekiri kwamba mchezo dhidi ya Burkina Faso ambao ni wa pili kwao wa Kundi D wa mchuano wa Mataifa ya Afrika ulikuwa mgumu.

Baghdad Bounedjah alifunga dakika za mwisho akiisawazishia Algeria na kuambulia pointi moja.

Belmadi ambaye alifurahishwa na matokeo ya timu yake katika mchezo huo alisema mchezo ulikuwa mgumu sana, lakini akaongeza kuwa ameridhika na matokeo.

"Nimeridhika sana na walichotoa uwanjani leo (juzi). Tuliiruhusu Burkina Faso kutawala zaidi kipindi cha kwanza, lakini tuliingia kipindi cha pili vizuri zaidi kwa hiyo tumeridhika na nimeridhika na sare. Ilikuwa mechi ngumu na timu ngumu, lakini tukatoka sare, tutaichukua kwa sasa.

"Timu ya Burkina Faso iliweka presha na nguvu nyingi katika mechi hii, hakuna kilichokuwa rahisi kwetu dhidi ya timu ngumu sana, hivyo tutaangalia mbele kwa pointi na kuvuka hatua hii ya makundi."

Algeria, ambao bado wanasaka ushindi wao wa kwanza kwenye michuano hiyo mwaka huu, watacheza mchezo wao wa mwisho dhidi ya Mauritania kesho, Jumanne katika Uwanja wa Paix mjini Bouake.

Belmadi aliongeza kuwa ameona makosa ya timu yake na ataimarika katika mchezo wao wa mwisho wa kundi hilo.

"Nimeona makosa tuliyofanya na nitayatumia kuboresha mechi yetu ya mwisho ya kundi.

"Tungeweza kukatishwa tamaa na kuwa na wasiwasi, lakini tulihakikisha tunafika kwenye mchezo wa pili tukiwa na mawazo bora zaidi. Nina hakika na wachezaji hawa tutafika mbali katika mashindano haya."



HABARI MICHEZO

# KILIMANJARO PREMIUM LAGER MARATHON YAZINDULIWA MOSHI

**Na Mwandishi Wetu**

TOLEO la 22 la Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon 2024, limezinduliwa katika Hoteli ya Salinero mjini Moshi, Kilimanjaro, jambo ambalo linaashiria wazi kwamba siku ya tukio hilo linalotarajiwa kufanyika Februari 25, mwaka huu limekaribia.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro wakati wa uzinduzi huo Ijumaa iliyopita, Nurdin Babu, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Tixon Nzunda, aliwapongeza waandaji wa mbio hizo kwa hatua iliyofikia hadi sasa tangu kuanzishwa kwake hasa kwa mchango wake katika kukuza utalii wa michezo na uchumi wa Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

"Tunajivunia mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon kwani zimeonekana kuwa moja ya matukio makubwa ya kimataifa katika ukanda huu kwa kuwakutanisha washiriki zaidi ya 12,000 na idadi kama hiyo ya watazamaji kutoka zaidi ya nchi 56 ambao wote hawa ni watalii watarajiwa," alisema na kuongeza, hili ni tukio kubwa sana na muhimu kwa taifa.

Nzunda aliendelea kusema kuwa hakuna mashindano mengine yanayoweza kufikia Kilimanjaro Marathon kwa maana ya matokeo yake katika kukuza uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

„Tumekuwa tukiandaa mbio za marathon kwa miaka 22 sasa na jumuiya ya wafanyabiashara itakubaliana nami kwamba kwa kawaida wakati wa mbio hizi ni msimu wa biashara aina mbalimbali mkoani hapa kukua ikiwa ni pamoja na hoteli zote na nyumba za kulala wageni kufanya biashara kubwa," alisema.

Aliongeza, "nitoe wito kwa wafanyabiashara wote kuzingatia ubora wa bidhaa zao pamoja na huduma watakazotoa ili kuhakikisha wageni wanapata thamani ya fedha watakazotumia".

"Nichukue fursa hii kuwapongeza wadhamini wote wa mbio hizi wakiongozwa na Kilimanjaro Premium Lager (mdhamini mkuu) na Tigo- Km 21 (Half Marathon), Gee Soseji wanaodhamini Km 5 (Fun Run) kwa mchango wenu mkubwa.

@Pia wadhamini wenza ambao ni Simba Cement, Kilimanjaro Water, TotalEnergies, CRDB Bank na TPC Sugar, pamoja na washirika rasmi ambao ni pamoja na Garda World, CMC Automobiles, Salinero Hotels na wasambazaji - Kibo Palace Hotel na Keys Hotel; bila ya nyinyi isingekuwa rahisi kufanikisha mbio hizi," alisema, huku akitoa wito kwa washiriki wa Kitanzania kujiandaa vema ili kuhakikisha zawadi nyingi zinabaki nyumbani.

Kwa upande wa Meneja wa Kampuni ya Bia Tanzania, Kanda ya Kaskazini Mashariki, Neema Patrick, alisema wanajivunia kupitia Kilimanjaro Premium lager, kudhamini hafla hiyo kwa miaka 22 iliyopita na kuwa miongoni mwa udhamini wa muda mrefu nchini, ambapo mbio hizo zimeendelea kuchangia utalii na utamaduni wa Mtanzania kwa ujumla.

Alisema TBL imetenga Sh. milioni 28 ikiwa ni zawadi ya fedha huku washindi wa kwanza katika kitengo cha wanaume na wanawake wakitarajiwa kupata zawadi ya Sh. milioni 4 kila mmoja.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Maino, alisema,"tunayo furaha kubwa kuwa wadhamini wa mbio za Tigo Half Marathon kwa mwaka wa tisa mfululizo. Tigo Half Marathon inawahusisha washiriki zaidi ya 6,000 kwa wakati mmoja wakiwamo wanariadha wa daraja la juu barani Afrika, hivyo napenda kuwajulisha kuwa zawadi katika kitengo hiki zimeongezeka".

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon zitafanyika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), na zimeandaliwa na Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa hapa nchini na Kampuni ya Executive Solutions Limited.




Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda (katikati), akikata utepe pamoja na Mkuu wa Masoko na Mauzo wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Neema Patrick (wa pili kushoto), wakati wa uzinduzi rasmi wa Kilimanjaro Premium Lager International Marathon 2024 katika Hoteli ya Salinero mjini Moshi Ijumaa iliyopita. Wengine kutoka kushoto ni Meneja Masoko wa Gee Soseji, Magreth Karua, Kaimu Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Mainoya na Mkurugenzi wa Hoteli ya Salinero, Ben Mengi. **MPIGAPICHA WETU**

# Dilunga amkaribisha Kichuya JKT Tanzania ikiingia kambini

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha JKT Tanzania kimeanza rasmi mazoezi na kambi kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kurejea kupigwa tena katikati ya mwezi ujao, huku kiungo Hassan Dilunga, akimkaribisha mchezaji mwenzake wa zamani wa Simba, Shiza Kichuya.

Kichuya ni mmoja wa wachezaji waliojiunga na kikosi cha JKT Tanzania kipindi cha dirisha dogo kilichomalizika Januari 15, akitokea Namungo FC.

Kikosi hicho kilianza mazoezi yake rasmi juzi kwenye Ufukwe wa Coco, Dar es Salaam baada ya mapumziko ya siku kadhaa.

„Shiza Ramadhani Kichuya, kona goli, karibu sana JKT Tanzania, karibu kwenye familia yetu, nakutakia kila la heri nakufahamu mwanangu, tena uko na wanao hapa, nipo mimi Ndemla (Said), hautakuwa mgeni, nadhani utauwasha kama kawaida yako," Dilunga alimkaribisha Kichuya ambaye alimjibu kwa kushukuru.

Dilunga ambaye kwa sasa ameanza mazoezi mepesi baada ya kuumia katika moja ya mechi ya Ligi Kuu, alijiunga na timu hiyo akitokea Simba.

Wachezaji hao wote wawili waliichezea Simba katikati ya miaka ya 2000 na kuipa mafanikio makubwa timu hiyo.

Akizungumza baada ya kukaribishwa kwenye kikosi hicho, Kichuya alisema atapambana ili kuhakikisha JKT Tanzania inatimiza malengo.

„Kikubwa naamini uwezo wangu, popote nitakapokuwa nacheza ndiyo kazini kwangu, nilikuwa Mtibwa nimetoka, Simba nimeondoka, Namungo pia sasa ni mchezaji wa JKT Tanzania nimekuja kuongeza nguvu na wanajeshi wenzangu ili kuipeleka timu ambapo mashabiki wa JKT Tanzania wanahitaji ifike, nina imani tufanya vema kutokana na usajili ambao viongozi wameufanya hasa huu wa maingizo mapya," alisema winga huyo.

## Simba wapitisha mambo 6

INATOKA UK. 24

**MO DEWJI ACHANGIA BILIONI 2.4/-**

"Katika bajeti ya fedha ya msimu wa 2022/23 Rais wa Heshima wa Simba Mohamed 'Mo' Dewji alituchangia kiasi cha Sh. bilioni 2.4 ambazo zilienda moja kwa moja kwenye kufanikisha kukusanya Sh. bilioni 15 ambazo zimetupa faida kwa kiasi kikubwa," alisema Kahumbu.

**USAJILI WATUMIA BILIONI 2.3/-**

"Kwenye usajili ambao tumeufanya msimu wa 2022/23 tulitumia kiasi cha Sh. bilioni 2.3 ambapo ni kwa wale wachezaji wapya ambao tuliwasajili kwa wale wa kimataifa kwa maana ya wachezaji wa nje na ndani," alisema.

**MISHAHARA WATUMIA BILIONI 4.8**

"Mishahara kwa wachezaji imetugharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.8, ikiwa ni bajeti ya msimu wetu wa fedha kwa mwaka 2022/23 hapa utaona ni kwa kiasi gani tunaweza kutumia fedha nzuri kuwalipa wachezaji wetu stahiki zao," alisema.

**BONASI KWA WACHEZAJI BILIONI 1.5**

"Kwenye michezo ambayo Simba inakuwa inacheza basi kuna bonasi kwa ajili ya timu na hapa inakuwa kwa upande wa timu zote ile ya kiume na ile ya kike, Simba Queens," alisema Suleiman Kahumbu, Mhasibu wa Simba," alisema Kahumbu.

Katika mkutano huo ulioanza saa 5:00 asubuhi, ulifunguliwa na Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, ambapo alisema Simba imeshafanya mambo mengi makubwa, yaliyopita, yanayofanyika sasa na mengine yanakuja.

„Lengo letu ni kujenga umoja. Mfano mtu anasema uwekezaji hauna faida wakati kabla ya uwekezaji mapato yalikuwa Sh. bilioni 1.6, mara baada ya uwekezaji yamepanda hadi Sh. bilioni 6.9.

„Afrika tulikuwa nafasi zaidi ya 80 kwenye ubora na sasa tupo nafasi ya saba. Tunataka ukosoaji wenye tija, kama mnakumbuka mlichanga pesa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja, pesa ile ilitumika kujenga ukuta wa uwanja wa Bunju na pesa zingine zilitumika kuimarisha kambi ya timu," alisema Mangungu.

Kwa upande wa mwakilishi wa mgeni rasmi, Nicolas Mihayo, ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo nchini (BMT), aliwapongeza Simba kwa kufuata maelekezo ambayo ilipewa kufanyia kazi katika mapendekezo ya marekebisho ya katiba.

"Hili ni jambo la mfano kwa timu zingine, kuzingatia yale yanayoagizwa na serikali, ambapo hivi karibuni Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, aliwaita Simba na kuwataka kufanyia kazi mambo kadhaa ya katiba yao na ninawapongeza na kuwatakia kila la kheri," alisema Mihayo.

# Michezo

Arteta awatoa hofu mashabiki kwa Rice UKURASA 21



Jumatatui Januari 22, 2024
Nipashe




Wanachama wa Klabu ya Simba wakisikiliza kwa makini kwenye mkutano mkuu wa klabu hiyo, uliofanyika ukumbi wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA SC WAPITISHA MAMBO 6

## ●●●Wanachama wapongezwa, wapinga kipengele kimoja cha mwakilishi...

**Na Saada Akida**

WAKATI Mwenyekiti wa Kamati ya Maboresho ya Katiba ya Klabu ya Simba, Hussein Kitta, akisema wanachama wamepitisha mambo sita ambayo walitakiwa kufanyia maboresho, uongozi wa klabu hiyo pia umeweka wazi bajeti yao ya msimu mpya wa fedha wa klabu hiyo wa mwaka 2023/24 wakiwa na malengo ya kukusanya jumla ya Sh. bilioni 25 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Simba jana ilifanya mkutano mkuu wa klabu hiyo jijini Dar es Salaam ambapo mambo hayo sita yaliyopitishwa ni mamlaka ya uteuzi ya bodi ya wadhamini baada ya kuteuliwa sasa wanatakiwa kuchaguliwa katika mkutano mkuu, kuweka wazi nafasi ya kupatikana kwa mwenyekiti, kuweka wazi malengo ya katiba na kuyaweka wazi malengo ya mkutano.

Kuwa na haja ya kupitisha kampuni inayoshiriki Hisa za Simba Sport Club na kuweka wazi hisa asilimia 99 inashikiliwa na bodi ya wadhamini na asilimia moja kwa Mwenyekiti ambaye anatakiwa kuwa wazi kuwa ni wanachama na kipengele cha sita ni mwakilishi mmoja wa wanachama katika mkutano mkuu.

Kitta alisema wanachama wamekataa kupitisha kipengele kimoja kinachoeleza kutoa mwakilishi wa mwanachama katika mkutano mkuu.

„Hicho kipengele tuliambiwa tukiweke kulingana na namna ya kuendesha mikutano yetu, lakini wanachama wamekikataa, kutokana na hilo ni sehemu ya mapendekezo tu tuliopewa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambayo haikuwa na ulazima,“ alisema Kitta.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Ushauri wa Klabu ya Simba, Geofrey Nyange Kaburu, amempongeza Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu kwa kuendesha mkutano vizuri na kufuata matakwa ya wanachama.

Alisema mkutano ulikuwa mfupi wenye ajenda nzuri zilizo na mafanikio kwa klabu huku akisisitiza kuwa katiba inatambua mahitaji ya wanachama, hivyo kupewa nafasi ya kusikilizwa ni jambo zuri.

"Pia Baraza letu limeingizwa kwenye katiba ya klabu hivyo tutakuwa tunashauri kwa mujibu wa katiba kwa sababu tayari tunatambulika.

„Mbali na sisi kutambulika kikatiba rasmi mwenyekiti wa klabu kapewa nafasi maalum kwa mujibu wa katiba kusimama kwa ajili ya wanachama," alisema Kaburu.

Katika hatua nyingine uongozi wa klabu hiyo umeweka wazi bajeti ya msimu mpya wa fedha wa klabu hiyo kwa mwaka 2023/24, kuwa na malengo ya kukusanya jumla ya Sh. bilioni 25 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Akizungumza kwenye mkutano huo mkuu, Mhasibu wa klabu hiyo, Suleiman Kahumbu, alisema: „Bajeti kwa mwaka 2023/2024 klabu imepanga kukusanya kiasi cha Sh. 25,930,722,300, lakini imepanga kutumia kiasi cha Sh. 25,423,997,354. Hivyo tutabaki na mapato ya ziada ya Sh. 506,724,946".

"Aidha, mapato yote hayo yanapatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ndani ya timu hiyo kama fedha ya mdhamini, haki za matangazo, mapato ya mlangoni, uuzwaji wa jezi, wadhamini wadogo wadogo na kushiriki katika michuano ya AFL ambayo imechangia kwa asilimia kubwa kuweza kupata mapato makubwa kwa klabu yetu msimu huu," alisema.

INAENDELEA UK. 23

## Wachezaji Yanga walilia mashabiki

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akitarajia kubadilisha programu ya mazoezi wiki hii kutoka ya ufukweni na kurejea uwanjani, wachezaji wa timu hiyo wamesema 'wamemisi' sana shangwe, kelele na furaha za mashabiki wao.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam, wachezaji Clement Mzize na Maxi Nzengeli wamesema tangu mechi za Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa na kumaliza Kombe la Mapinduzi na kuwa kwenye mapumziko, wamepooza na wameanza kuwakumbuka tena mashabiki ambao huwafuata popote waendapo, wakiwaahidi makubwa zaidi watakaporejea uwanjani.

Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa kwa sasa imesimama kupisha fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast.

„Tumewamisi' mashabiki wetu, wao hutufuata popote tuendapo, wanatushangilia kwa nguvu zote na kutupa morali, furaha na kujituma kuipambania nembo ya klabu, leo hii hatuwaoni kwa sababu mechi zimesimama na sisi tulipata mapumziko kidogo, nina imani tutakutana tena na tutakuwa na wakati mzuri kwa mara nyingine," alisema kiungo mshambuliaji Maxi Nzengeli raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo.

Naye straika Clement Mzize alisema ana hamu tena ya kuwaona mashabiki uwanjani na anajua pia hata wanachama na mashabiki wao pia wana hamu ya kuwaona wachezaji wao.

„Wananchi, wanachama na mashabiki wa Yanga, wana hamu ya kutuona tukicheza na kupambana uwanjani, ‚wametumiss na tumewamiss' sana mashabiki wetu, tulikuwa nao pamoja, tuliwapa furaha na kushangilia kwa pamoja, naamini tutakuja kivingine tena, yale yamepita, tutakuja mara mbili zaidi ya mwanzo," aliahidi Mzize.

Wakati huo huo, kocha Gamondi ambaye wiki nzima alikuwa akiwafua wachezaji wake kwenye fukwe za Coco na kuwapeleka gym, anatarajia kubadilisha programu na kuhamia uwanjani.

Meneja wa timu hiyo Walter Harrison, alisema mabadiliko hayo ya benchi la ufundi yatafanyika baada ya kuridhishwa na mazoezi ya awali waliyowapatia wachezaji.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >